**Jafo** awaweka wakurugenzi wanne matatani

UKURASA 4



**Bucha** nyamapori 'yachangamkiwa' wengi wakosa kitoweo

UKURASA 5


Nipashe TESA

Jumanne Desemba 22, 2020 TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

Ukurasa 12

Waja na ujasiriamali kuwaokoa mabinti na uhalifu wa kingono

Ukurasa 13

TAS inavyopambana na saratani ya ngozi, yasambaza mashine kutoa tiba

Ukurasa 14

Dk. Hellen Kijo - Bisimba atoa ushuhuda unaochoma, kuonya na kutaka kazi zaidi

TEKNOLOJIA

NA SABATO KASIKA

TEHAMA MAHAKAMANI

▪Kesi kuendeshwa bila majalada

▪Si lazima kuhudhuria kortini

NI ukweli usiopingika kwamba dunia imebadilika, hivyo mambo mengi yanafanyika kulingana na sayansi na teknolojia na ubunifu zaidi unaosukumwa na matumizi ya kompyuta au simu za mkononi zikiwa injini ya kufanikisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Ni zama mpya ya kimawasiliano na kufanyakazi kumerahisika na kuimarika kutokana na kukua kwa teknolojia zenye miundombinu isiyohitaji kuunganisha nyaya marufu kama 'wireless', na mawimbi ya mawasiliano yakitua kwenye simu na kompyuta kwa njia ya masafa ya Wi-Fi (wai-fai).

haki hauwezi kutenganishwa na matumizi ya bora ya TEHAMA na kwamba kwa msingi huo, anaamini mfumo huo ni nyenzo muhimu katika kuwezesha utoaji haki kwa wakati na kusogeza huduma za mahakama karibu zaidi na wananchi.

"Hivyo mahakama na wadau wake hawawezi kubaki nyuma kwani mapinduzi ya TEHAMA yameshakubalika na dunia iliyoshindani kuwa ni muhimu katika utoaji huduma za haki," anasema Jaji Kiongozi.

mahakama," anasema na kuongeza kuwa mwelekeo wa sasa katika matumizi ya TEHAMA ni kuwa mahakama isiyotumia karatasi.

MANUFAA YA TEHAMA

Inaelezwa kuwa mfumo huo una manufaa mengi, kuanzia kutunza kumbukumbu, kama njia ya kupunguza mrundikano wa karatasi na kuwezesha ofisi kuwa na kompyuta chache zenye uwezo wa kutunza kumbukumbu.

UKURASA 11

# Nipashe

Jumanne Desemba 22, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580437

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



UKURASA 2

# Vijiji vyote kuunganishiwa umeme 2021

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**NCHEMBA AAGIZA TAARIFA ZA WANANCHI KURASIMISHWA**

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Mwigulu Nchemba, ameagiza wananchi ambao...

## Mahakama yaipa Symbion siku 14 kulipa wafanyakazi

UKURASA 5

Scan Hapa



Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store



Baadhi ya wakazi wa jijini Dar es Salaam, wakinunua nguo na vitu mbalimbali katika Mtaa wa Kongo jana, kwa ajili ya maandalizi ya sikukuu ya Krismasi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Matukio yaliyotikisa nchini

UK. 2

**MICHEZO** NTIBAZONKIZA AUTAJA UBINGWA YANGA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Nchemba aagiza taarifa za wananchi kurasimishwa

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Mwigulu Nchemba, ameagiza wananchi ambao taarifa zao zimesajiliwa kwenye mfumo wa serikali kurasimishwa ili kuwaondolea usumbufu wa kujisajili kila mara.

Nchemba ametoa agizo hilo jana jijini Dar es Salaam wakati alivyofanya ziara ya kukutana na viongozi wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) na wafanyakazi kuhusu utendaji kazi.

Aliitaka RITA kuhakikisha inaongeza nguvu katika mifumo ya taarifa ya namna ya kurasimisha ili wananchi wasiendelea kusumbuka.

"Kwa sababu serikali ni moja kuna taarifa nyingi tayari zimeshafanyiwa kazi na kutambulika rasmi kuwa ni taarifa za serikali ni vyema tukaendelea kuzitumia kwa kuwa vyanzo vyake ni vya serikali na tutazigakuwa hizi ni taarifa za usajili," alisema Nchemba.

"Kwa mfano kuna vyanzo vingi vya taarifa ni rasmi watu ambao wamepata vyeti vya uraia hiyo ni ofisi rasmi ya serikali, watu ambao wamepata hati za kusafiria kuna maeneo mengine kama kwenye shule zetu zinaonyesha takwimu ama maeneo ya chanjo ama kwenye mifuko ya hifadhi," alisema.

Waziri alisema watu hao ambao taarifa zao zipo kwenye ofisi za serikali ni vizuri zikarasimishwa badala ya kuwataka kila wakati kujisajili kwenye ofisi tofauti.

Alisema kitendo hicho kitasaidia upatikanaji wa taarifa sahihi za usajili katika nchi na kuondoa tatizo la ofisi kurushiana majukumu.

"Unakaa ofisi moja ya serikali inakuwa na majukumu ambayo ni ya ofisini nyingine ya serikali hii nayo inafanya ofisi kufanya kazi kwa kushirikiana na kuwaondolea wananchi wetu usumbufu wa kusajili kila wakati, yaani ukihitaji jambo fulani unaanza usajili upya ukihitaji jingine unaanza usajili upya hii ni usumbufu," alisema.

Alisema haipendezi mtu ambaye anakitambulisho cha uraia halafu akaenda eneo jingine kuanza kuandikishwa upya na kuishauri RITA kuliangalia suala hilo.

Alitaka waandikishe kwa uangalifu na taarifa hizo zisomeke sawa na taasisi nyingine.

Vile vile, alisema utaratibu wa utoaji vyeti umekuwa na udanganyifu mwingi kuliko wa kutoa taarifa kwa uhalisia wa tukio.

"Mtoto anavyozaliwa hapa hakuna namna ya kudanganya, lakini vyeti vinavyotolewa kutokana na uhitaji kuna udanganyifu mwingi mtu mmoja anaweza akawa na vyeti hata vitatu, akitaka kuoa anatoa cheti chenye umri mwingine kama ni mchezaji akitakiwa Serengeti boys, anatoa umri unaotakiwa kujiunga na Serengeti boys haya ni madhara ya kutoa cheti kutokana na uhitaji," alisema Mwigulu.

"Vyeti wanavitengeneza tena wanasema naenda kachongesha kwenye utoaji wa vyeti unaweza kutoa hata kwa ambao siyo raia, hii ni madhara kwa nchi lazima tuangalie maslahi ya nchi," alisema.

Waziri Nchemba alisema ikigundulika mtu ametoa cheti kwa raia ambaye siyo Mtanzania, aliyehusika atachukuliwa hatua kali kwa mujibu wa sheria.

Alisema taasisi hiyo ni muhimu kwa serikali katika kupanga mambo yake na kwamba ni lazima ijiepushe na utoaji vyeti vya kuzaliwa kwa watu ambao siyo raia wa Tanzania.

Askari Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Constable Eniko Kayombo (aliyelala chini), akikagua basi la abiria kwa usalama zaidi, kulia ni Constable Essau Tindwa, ukaguzi uliofanyika katika kituo cha mabasi Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIARAJI MSALA**



## Zaidi ya vijiji 2,000 kupata umeme 2021

**Na Thobias Mwanakatwe**

HATIMAYE ahadi ya Rais John Magufuli aliyoitoa wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu kwamba kila kijiji kuwa na nishati ya umeme ifikapo mwaka 2022 imeanza kutekelezwa, baada ya waziri mwenye dhamana kutoa tamko.

Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, ameeleza kuwa ifikapo Februari 5, mwakani, makandarasi watasambaa nchi nzima kwa ajili ya kuanza kazi ya kusambaza huduma hiyo kwenye vijiji vyote.

Dk. Kalemani aliyasema hayo juzi, katika kipindi cha Papo kwa Papo kinachoendeshwa na Katibu wa Siasa, Itikadi na Uenezi, Humphrey Polepole.

Hatua hiyo ni mojawapo ya ahadi ya Rais John Magufuli aliyoitoa wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu akiwa katika mikoa mbalimbali.

Kwenye kampeni hizo, Rais Magufuli alisema ifikapo mwaka 2022, vijiji vyote ambavyo havijafikiwa na huduma ya umeme, vinafikiwa.

Rais Magufuli alisema wakati anaingia madarakani mwaka 2015, idadi ya vijiji vilivyokuwa na umeme nchini vilikuwa 2,018, na kuwa hadi mwaka huu idadi hiyo imeongezeka na kufikia vijiji 9,570, huku vikisalia 2,600.

Akiwa katika kipindi hicho, Dk. Kalemani alisema kazi ya kusambaza umeme katika kipindi cha miaka mitano iliyopita imeshafanyika katika vijiji takribani 10,000 kati ya 12,280 vilivyopo nchini na vilivyobaki ni 2,270.

"Tutahakikisha maeneo yote ambayo hayajafikiwa na umeme ifikapo Desemba 2022 vijiji nchi nzima vitakuwa na umeme, nasisitiza gharama za kuunganishiwa umeme ni shilingi 27,000, mwananchi haruhusiwi kulipia gharama za nguzo wala transifoma," alisema.

Rais Dk. John Magufuli, Novemba 13, 2020 akizindua Bunge la 12 alisema kwenye miaka mitano ijayo, serikali imepanga kufikisha umeme kwenye vijiji vyote ambavyo bado havijafikishiwa huduma hiyo.

Rais Magufuli alisema serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya nishati na pia kuboresha upatikanaji wa huduma na kazi inayofanyika ni kukamilisha ujenzi wa Bwawa la kufua umeme la Nyerere litakalozalisha megawati 2,115.

# Jeshi la Polisi lataja matukio yaliyotikisa nchini

**Na Elizabeth Zaya**

WAKATI zikiwa zimebaki siku 10 kuuaga mwaka 2020, Jeshi la Polisi limeorodhesha matukio ambayo yalitikisa nchi na kukabiliana nayo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotumwa jana kwa vyombo vya habari na Kamishna wa Operesheni na Mafunzo, Makao Makuu ya Jeshi hilo, CP Liberatus Sabas, matukio hayo ni ya wanafunzi kuacha shule na kujiunga katika makundi ya uhalifu ambao baadhi yao baada ya kukurupushwa walikimbilia nchi jirani.

Matukio mengine ni ya shule kuungua moto, mauaji yaliyosababishwa na wivu wa mapenzi, wananchi kujichukulia sheria mkononi, unyang`anyi wa kutumia silaha, ajali za barabarani ambazo hata hivyo, kwa mwaka huu zimepungua kulinganisha na mwaka jana.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa matukio hayo yalitokea kuanzia Januari hadi Novemba, mwaka huu.

### WANAFUNZI

Akizungumzia suala la wanafunzi kujiunga na uhalifu, Kamishna Sabas alisema kumekuwapo na wimbi kubwa la watoto kuacha shule na kwenda kujiunga na makundi ya kihalifu na miongoni mwa wahalifu hao ni waliokuwa wilayani Kibiti.

"Miongoni mwa wahalifu hao ni wale waliokuwa Kibiti na hatimaye baada ya kupigwa na Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, walikimbilia nchi jirani ya Msumbiji," alisema Kamshina Sabas na kuongeza:

"Jeshi la Polisi nchini linawaomba wazazi na wakazi kufuatilia nyendo za watoto wao, kuwalinda na kufuatilia mienendo yao, na wananchi nao wanatakiwa kuchukua tahadhari wakati huu wa kuelekea sikukuu za mwisho wa mwaka."

### SHULE KUUNGUA

Kamishna Sabas alisema matukio ya shule kuungua moto yalitikisa mwaka huu, huku akitaja baadhi ya sababu za matukio hayo kuwa ni migogoro katika shule hizo na uzembe.

"Miongoni mwa matukio yaliyoshika kasi na nafasi kubwa mwaka huu ilikuwa ni kuungua kwa majengo ya shule na hii imetokana na sababu ambazo ni hitilafu za umeme, migogoro ya shule na uzembe," alisema Kamishna Sabas.

Alisema jumla ya shule zilizoungua moto ni 31, huku za watu binafsi na taasisi za kidini zikiwa 20 na za serikali 11.

### WIVU WA MAPENZI

Kamishna Sabas alisema kwa kiasi kikubwa mauaji yanayotokea kwa sasa yanasababishwa na wivu wa mapenzi na wananchi kujichukulia sheria mkononi.

### UNYANG'ANYI WA SILAHA

Akizungumzia matukio ya unyang'anyi wa kutumia silaha, alisema kwa mwaka huu jeshi hilo limefanikiwa kupunguza makosa ya ujambazi wa aina hiyo kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

"Mwaka jana kuanzia Januari hadi Novemba, makosa yalikuwa 378 na mwaka huu hadi Novemba yalikuwa 273," alisema Kamishna Sabas.

### AJALI ZA BARABARANI

Kwa upande wa ajali za barabarani, Kamishna Sabas, alisema kwa mwaka jana zilikuwa 2,722, zilizosababisha vifo ni 1,117 wakati waliofariki kutokana na ajali hizo ni watu 1,329 huku majeruhi wakiwa 2,717.

Alisema kwa mwaka huu hadi Novemba ajali zilikuwa 1,800, waliofariki kutokana na ajali hizo ni 1,158 na majeruhi ni 2,089.

TANGAZO

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

LATRA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini

## TAARIFA KWA UMMA YA KUKANUSHA HABARI ZA KUPOTOSHA ZILIZOSAMBAA KUHUSU MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI (LATRA)

| NA | KUHUSU | HABARI YA KUPOTOSHA | UKWELI |
|---|---|---|---|
| 1 | Ukaguzi wa leseni za usafirishaji. | Maofisa wa LATRA wanakamata magari ya watu yasiyofanya biashara sehemu mbalimbali nchini. | LATRA hutoa leseni kwa magari ya biashara. Hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha 5 (1)(b) cha Sheria Na. 3 ya mwaka 2019. Hivyo, ukaguzi hufanywa kwa magari ya biashara kuhakikisha watoa huduma wanazingatia takwa hili la kisheria. Wafanyakazi wa LATRA wanazingatia sheria hiyo. |
| 2 | Huduma kwa Wateja | Tukio la Afisa wa LATRA mkoa wa Lindi kugombana na dereva wa lori linaashiria kuwa hawana huduma nzuri kwa wateja. | Tukio hili haliwakilishi utendaji wa wafanyakazi wa LATRA. Wafanyakazi wa LATRA hufanya kazi kwa weledi na wamepata mafunzo ya Huduma kwa Wateja. Vilevile, kila mwaka, hupewa mafunzo ya Sheria, Kanuni na Miongozo ya utendaji kazi.<br><br>Kwa kuonyesha kuwa kitendo hicho hakikubaliki, LATRA ilimsimamisha kazi mfanyakazi huyo ndani ya saa 24. |
| 3 | Lengo kuu la Mamlaka | Lengo kubwa la LATRA si kuwalinda wasafirishaji, bali kuwakandamiza kutokana na kanuni zao ngumu. | Kwa mujibu Kifungu cha 6 cha Sheria ya LATRA Na. 3 ya mwaka 2019 jukumu kuu la LATRA ni kuboresha maisha ya Watanzania kupitia sekta ya usafiri ardhini kwa;<br>· kuimarisha ushindani na usalama,<br>· kulinda maslahi ya mtumiaji wa huduma na watoa huduma wenye ufanisi.<br>· Vilevile, kuhakikisha uwepo wa huduma za usafiri zenye uhakika na<br>· kutoa elimu kwa umma.<br><br>Changamoto iliyopo ni kuwepo kwa wasafirishaji wachache wasiotaka kutii sheria. |
| 4 | Ushirikishwaji katika Kutunga Kanuni za LATRA | Wakati wa utungwaji wa Kanuni mpya za LATRA za mwaka 2020 wasafirishaji hawakushirikishwa. | Wizara yenye dhamana na Uchukuzi, ikishirikiana na LATRA ilifanya mikutano kupata maoni ya Wadau mwezi Agosti, 2019. Mikutano hiyo ilifanyika kikanda katika mikoa ya Dar es Salaam (2), Arusha, Mwanza, Mbeya, na Dodoma.<br><br>Wasafirishaji walishiriki na maoni yao yalizingatiwa. |
| 5 | Zabuni za vifaa vya kufuatilia mwenendo wa mabasi (VTS) | Mchakato wa kupata Kampuni moja iliyopewa zabuni ya kuuza vifaa vya ufuatiliaji magari (Vehicle Tracking System) haukuwa sahihi. | Kampuni zinazofunga vifaa vya ufuatiliaji wa mwenendo kwenye mabasi ni nne (4). Ambazo ni<br>· Tera Technologies and Engineering Ltd,<br>· Easy Track,<br>· ICTpak na<br>· U-Track.<br><br>Kampuni hizi zilipatikana kwa njia ya ushindani kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi ya Umma kupitia mfumo wa TaNEPS.<br><br>Sababu ya kuwa na kampuni zaidi ya moja ni kuweka ushindani na kuwapa wasafirishaji wigo wa kuchagua kampuni wanayoiona inafaa zaidi. |
| | | VTS inatumika na LATRA kama kitega uchumi. | Mamlaka haipati fedha yoyote kutokana na VTS. Gharama hulipwa kwa kampuni za kufunga vifaa kwa ajili ya kununua kifaa na kulipia gharama za usimamizi za kila mwezi pamoja na mawasiliano (data). |
| 6 | Udhibiti wa mwendokasi hatarishi wa mabasi. | Basi lenye VTS linapozidisha mwendokasi uliopangwa wa kilomita 80 kwa saa, huachwa liendelee. Mwisho wa mwezi mmiliki anatozwa faini kulingana na mara ngapi dereva alizidisha mwendo. | Basi likizidisha mwendokasi kingo'ra ndani ya basi hulia kumtahadharisha dereva kupunguza mwendo. Aidha, kila basi lina speedomita inayomwezesha dereva kuona spidi ya gari. Vilevile, wamiliki wamepatiwa akaunti zinazowawezesha kuyaona mabasi yao kupitia simu zao za mkononi na kompyuta. Pale dereva na mwenye basi wanaposhindwa kuwajibika ndipo Mamlaka uingilia kati na kuchukua hatua ya kumtaarifu mmiliki na kuchukua hatua dhidi ya dereva na si mmiliki.<br>Na kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa LATRA haiwachukulii hatua madereva kutokana na amri ya Mahakama Kuu. |
| 7 | Kanuni za LATRA | Kanuni za LATRA zina nguvu kubwa na zinaingiliana na majukumu ya Sheria ya Usalama Barabarani na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) | Kifungu cha 5 (1)(f) cha Sheria Na. 3 ya mwaka 2019 kinaipa LATRA jukumu la kudhibiti ubora wa vyombo vya usafirishaji ardhini. Jukumu hili ni tofauti na jukumu la Sheria ya Usalama Barabarani Sura 168.<br><br>Aidha, LATRA hakusanya levi kwa mujibu ya Kifungu Na. 35 (2) cha Sheria Na. 3 ya mwaka 2019. Hivyo, kutoingiliana kimajukumu na TRA. |
| 8 | Tozo ya Levi kwa waendesha Bodaboda | LATRA wanataka kuwasajili bodaboda waanze kuwatoza asilimia moja (1%) ya mapato ghafi. | LATRA inatoa leseni za bodaboda toka mwaka 2010 na haijawahi kuwataka bodaboda kulipa levi ya asilimia moja (1%).<br>LATRA ilipewa jukumu hili kupitia marekebisho ya Sheria ya Leseni za Usafirishaji ya mwaka 2009 yaliyofanywa kwa lengo la kurasimisha usafiri wa pikipiki kibiashara. |
| 9 | Maagizo ya Mh. Waziri Mkuu | Juni 30, 2019, Waziri Mkuu alielekeza kusitisha malipo ya vifaa vya ufuatiliaji magari (VTS). | Mh. Waziri Mkuu alisitisha malipo na kuitaka LATRA isimamie majadiliano kati ya wasafirishaji na watoa huduma kuangalia uwezekano wa kupunguza viwango vya ada za kila mwezi. Agizo hili lilitekelezwa na LATRA kwa kuwakutanisha wazabuni na wasafirishaji ambapo walifikia muafaka wa viwango vya kulipana kwa kila mwezi. |
| 10 | Ada ya Leseni za Malori | LATRA imepandisha ada ya stika kutoka Tshs 7,000 mpaka Tshs 185,000 kwa lori na Tshs 185,000 kwa trailer. Faini ni Tshs 500,000 kwa kila kosa. | Ada ya juu kabisa kwa leseni za malori ni Sh. 120,000.<br><br>Aidha, kuendesha gari la biashara bila ya leseni ni kosa kwa mujibu wa Kanuni ya 23 ya Kanuni za leseni za Usafirishaji (Magari ya Mizigo), za mwaka 2020 (Kiambatishi VI). Mtu atakaye dhibitika kufanya kosa atatozwa faini ya kati ya shilingi laki 2 na isiyozidi laki 5, au kifungo cha kuanzia miezi mitano na isizidi mwaka mmoja au vyote kwa pamoja. Na endapo mmiliki atakiri kosa na kukubali kulipa faini papo kwa hapo, hulipa nusu ya faini hiyo ambayo ni Sh. 250,000.<br>Hata hivyo, kanuni zinampa nafasi mwenye gari kukata leseni mwezi mmoja kabla ya leseni kuisha ili kuepuka usumbufu na leseni hiyo inaweza kukatiwa mahali popote nchini. |
| 11 | Kauli ya Mkurugenzi Mkuu wa LATRA kuhusu Tiketi Mtandao (e-Ticketing) | Mkurugenzi Mkuu wa LATRA kutoa kauli ya kusitisha matumizi ya mfumo wa Tiketi Mtandao wa National Internet Data Centre (NIDC). | Maneno hayo hayakutolewa na Mkurugenzi Mkuu wa LATRA. Aidha, LATRA haina uwezo wa kusimamisha matumizi ya mfumo wa Tiketi Mtandao kwani Mfumo huo umeanzishwa na Serikali kwa malengo mapana. |
| 12 | Madaraja ya leseni za udereva na vyeti vya uwezo | Majukumu ya Kifungu cha 19, 20, 23, 24 na 25 vya Sheria ya Usalama Barabarani kuhusu leseni ya udereva yanaingiliana na jukumu la LATRA kupitia kifungu cha 5(1) cha Sheria ya LATRA Na. 3 ya mwaka 2019. | Sheria ya LATRA Na. 3 ya mwaka 2019 inaipa Mamlaka uwezo wa kuthibitisha madereva wa kuendesha magari ya biashara ambayo yanadhibitiwa na Mamlaka. Utaratibu huo sio mgeni na una lengo la kuongeza usalama wa vyombo hivyo na ubora wa huduma zinazotolewa. |

## RC aagiza kukamatwa wajumbe tuhuma upotevu mbolea

**Na Vicent Tiganya,** TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, ameagiza kukamatwa kwa wajumbe wa Bodi ya Chama Kikuu cha Ushirika Milambo, mkoani Tabora na baadhi ya watendaji kwa tuhuma za upotevu wa mbolea ya tumbaku mifuko 462, ikiwa na thamani ya Sh. milioni 55.

Alitoa agizo hilo jana, baada ya kutembelea ghala la chama hicho la kuhifadhi pembejeo na kukuta halijavunjwa, huku mbolea ikipotea katika mazingira ya kutatanisha.

Akiwa katika ghala hilo, Dk. Sengati alisema, anaunga mkono hatua iliyochukuliwa na Mrajisi wa Vyama vya Ushirika, Dk. Benson Ndiege, ya kuvunja bodi hiyo na kinachofuata ni kuhakikisha wahusika wa upotevu huo wanakamatwa, wanarudisha mbolea na kupelekwa mahakamani.

Pia, aliagiza Meneja Mkuu wa chama hicho, Leaky Madale na Mtunza Ghala, Sara William nao wachukuliwe kwa uchunguzi wa polisi.

## Pinda ataka kero za elimu ziondolewe

**Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, amekitaka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), kuangalia namna ya kushirikiana na mamlaka mbalimbali za elimu, ili kuondoa kero zilizopo na kuboresha elimu.

Pia, amekitaka chuo hicho kusambaza programu ya mradi wa vituo vya elimu ya awali katika maeneo mbalimbali nchini kutokana umuhimu wake kwa jamii.

Aliyasema hayo jana, wakati wa mahafali ya kwanza ya walimu wa stashahada ya awali ya shule za msingi na sekondari waliohitimu katika chuo hicho, chini ya ufadhili wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Walimu Duniani.

Pinda alisema elimu hiyo ni muhimu kwa jamii kwa sababu walimu wa shule hizo ndiyo waanzilishi wa msingi mzuri kwa wanafunzi waliopo katika hatua hiyo.

Alisema kuna kila sababu ya chuo cha OUT kuendelea kuisambaza programu hiyo katika mikoa mingine.



Baadhi ya mawakili wapya 166 waliopata kibali cha kuhudumu kazi hiyo, wakiwa katika sherehe iliyofanyika kwenye viwanja vya Karimjee, jijini Dar es Salaam jana, na kuhudhuriwa na Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Jafo awaweka matatani wakurugenzi 4

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, amemwagiza Katibu Mkuu TAMISEMI, Joseph Nyamhanga, kuwachukulia hatua wakurugenzi wa halmashauri nne, walioshindwa kutoa ruhusa kwa wakuu wa shule za sekondari kuhudhuria mkutano mkuu wao wa mwaka.

Waziri Jafo aliwataja wakurugenzi hao kuwa ni wa Halmashauri ya Msalala, Kahama, Kologwe na Sikonge.

Alitoa agizo hilo jana wakati alipokuwa akifungua Mkutano Mkuu wa mwaka wa Chama cha Wakuu wa Shule za Sekondari Tanzania Bara (TAHOSSA), unaofanyika jijini Dodoma. Alisema, mkutano huo ndiyo sehemu ambayo serikali inatumia kutoa maagizo kwa wakuu wa shule katika usimamizi wa masuala mbalimbali ya kielimu.

Vile vile, alisema serikali imetoa fedha nyingi kuboresha miundombinu ya elimu ambayo wasimamizi wakuu ni wakuu wa shule za sekondari na kufafanua ushiriki wao katika mkutano huo ni jambo la lazima.

"Kuna kiasi kikubwa cha fedha serikali imewekeza katika kuboresha miundombinu ya shule nchini na wasimamizi ni nyinyi wakuu wa shule, hivyo uwapo wenu hapa na sisi serikali tunapata fursa yakutoa maagizo yetu, lakini sasa kuna baadhi ya wakurugenzi wameshindwa kutoa vibali kwa wakuu wa shule," alibainisha Jafo.

Kutokana na hali hiyo, Waziri Jafo, alimwagiza Katibu Mkuu TAMISEMI, Mhandisi Joseph Nyamhanga, kuwachukulia hatua wakurugenzi hao haraka.

"Namwagiza Katibu Mkuu TAMISEMI, Nyamhanga kuhakikisha wakurugenzi hawa wanatoa maelezo kwanini wameshindwa kutoa ruhusa na hatua hizo zichukuliwe haraka," alisema Jafo.

Pia, aliwaagiza wakurugenzi wote wa halmashauri nchini kuhakikisha kuwa mwaka 2021, wanasimamia upimaji wa maeneo ya shule, ili kupata hatimiliki na kuondoa migogoro ya ardhi.

Alisema ni aibu kwa mkurugenzi kuwa na ofisa ardhi katika ofisi yake, lakini maeneo mengi ya shule hayajapimwa hali inayosababisha uvamizi wa maeneo na migogoro ya ardhi baina ya taasisi na wananchi katika maeneo husika.

Aidha, alisema katika mwaka wa fedha 2020/21, serikali imetenga zaidi ya Sh. bilioni 68 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 2,088.

"Tumetenga kiasi cha Sh. bilioni 42.3 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya maabara, ili kuwezesha vijana wetu wanaosoma masomo ya sayansi kujifunza kwa vitendo," alisisitiza Jafo.

Awali, Rais wa Chama cha Wakuu wa Shule Tanzania Bara (TAHOSSA), Vitaris Shija, alisema mkutano huo ni wa 15, kufanyika na kuiomba serikali kupima maeneo ya shule ili kuondokana na migogoro ya ardhi.

"Changamoto nyingine ndugu mgeni rasmi ni kutokana na shule nyingi kukosa uzio hali inayosababisha utendaji kazi kwa walimu kuwa katika mzingira yasiyo rafiki pamoja na wanafunzi wao."

Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE), Dk. Adolf Rutayuga, alisema wameshiriki katika mkutano huo kutokana na wateja wao wakuu kutoka katika shule za sekondari na kwamba watakuwa na fursa ya kukutana na wakuu wa shule pamoja na wadau wengine wa elimu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Global Education Link, Abdulmalik Mollel, ambao ni waratibu wa mkutano huo, alisema kuwa umekuwa na mabadiliko makubwa tofauti na miaka iliyopita.


COMPREHENSIVE COMMUNITY BASED REHABILITATION IN TANZANIA
CCBRT

## Tender Notice: Sale of Used Motor Vehicles

**Introduction**

Comprehensive Community Based Rehabilitation in Tanzania (CCBRT) is a locally registered non-governmental organisation providing specialised healthcare services operating in Dar es Salaam and Moshi, Tanzania. From its inception as a provider of community based rehabilitation, CCBRT has become the largest provider of disability and rehabilitative services in the country.

**Details**

CCBRT welcomes competitive bids for the sale of its used motor vehicles on 'AS IS' and 'WHERE IS' basis. The vehicles on sale by tender are as listed below and are available for viewing and inspection on week days from 21st December, 2020 from 8am to 2pm at the organizations premises situated, Off Kimweri Road, Msasani, Dar es Salaam, upon arrival call: 0767 123 482 or 0715 552 524.

1. Make Toyota, model Land Cruiser Hard Top, Year 2011, T327CAN.
2. Make Toyota, model Land Cruiser Hard Top, Year 2004, T401AKL.
3. Make Toyota, model Land Cruiser Hard Top, Year 2004, T405AKL.
4. Make Suzuki, model Jimmy Station wagon, Year 2004, T866ANH.
5. Make Toyota, model Coaster Bus, Year 1994, T847AWW.
6. Make Tata, model LP Bus, Year 2010, T412BVB.
7. Make Nissan UD, model MKB21OH Bus, Year 2011, T766CDP.
8. Make Nissan UD, model MKB21OH Bus, Year 2011, T774CDP.
9. Make Scania, model F114 Bus, Year 2009, T430CDQ.

**Content of the bid**

The bid must include the following information:

1. Name and surname, address, telephone number and e-mail address and physical location.
2. Description of the BID: The goods or services tendered must be described.

**How to submit bids**

Bids may be submitted:

a) In person and inside a sealed envelope, at CCBRT Hospital premises, Off Kimweri Road, Msasani, Dar es Salaam
b) By post, mail order etc. The envelope must be addressed as follows:

**Chief Executive Officer,**
**CCBRT**
**P.O.Box 23310**
**Msasani, Dar es Salaam**

160501

**Terms and Conditions of Sale**

1. The vehicles are sold strictly on 'AS IS' and 'WHERE IS' basis. CCBRT is not responsible for undertaking any repairs that may be required on the vehicles.
2. Deadline for the submission of the bids is 20th January, 2021, 12noon.

**IMPORTANT:** BIDS SUBMITTED AFTER THE DEADLINE WILL NOT BE ACCEPTED, REGARDLESS OF THE REASONS FOR THE DELAY.

## HABARI KITAIFA

# Bucha nyamapori 'yachangamkiwa', wengi wakosa nyama

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kutekeleza agizo la Rais John Magufuli, alililotoa wakati akizindua Bunge la 12 mwaka huu, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA), imezindua rasmi bucha la kuuza nyamapori katika Jiji la Dodoma.

Uzinduzi huo ulifanyika juzi katika Mtaa wa Chang'ombe jijini Dodoma na kushuhudia umati mkubwa wa watu wakinunua bidhaa hiyo.

Licha ya kuuzwa kwa Sh. 5,000 kwa kilo moja, wananchi wengi walikosa baada ya kuambiwa kuwapo kwa orodha ndefu ya majina ya watu walioweka oda mapema kununua nyama hiyo.

Mwenyekiti wa Bodi ya TAWA, Meja Jenerali mstaafu Hamisi Semfuko, alizindua bucha hiyo akiwataka Watanzania kutumia rasilimali zao kwa manufaa yao.

Hata hivyo, Semfuko alionya kufunguliwa kwa bucha hiyo kusisababishe uvunaji holela wanyamapori na kuahidi kufuatilia kila hatua kuona suala la ujangili linakomeshwa.

"Ninapofungua bucha hii kunatoa nafasi ya mabucha mengine kufunguliwa nchini, lakini natoa onyo kwa yeyote atakayetumia mwanya huu kufanya vitendo vya ujangili kwa kisingizio cha bucha, serikali ina macho makali lazima tutawashughulikia," alisema Semfuko.

Kadhalika, Semfuko alisema watakaofuata taratibu zote hakutakuwa na mzunguko wa kupata vibali vya uvunaji na uuzaji wa nyama hiyo na itauzwa kwa kufuata taratibu zote za serikali pamoja na miongozo ya afya.

Naye Kaimu Kamishna wa TAWA, Mabula Nyanda, alisema kufunguliwa kwa mabucha ya wanyamapori ni agizo la Rais John Magufuli, la kutaka Watanzania kunufaika na rasilimali zao.

Nyanda, alisema serikali itaboresha mfumo wa uuzaji nyamapori katika mabucha na ukaguzi utakuwa wa mara kwa mara ili kubaini kama kuna watu wanaingiza nyama hiyo kwa njia za panya, ili washughulikiwe kwa mujibu wa sheria.

Vile vile, alisema kwa sasa TAWA inaandaa mwongozo utakaowezesha watu kuwa na mashamba yao kwa ajili ya kufuga wanyamapori ambao watawatumia kuvuna na kuuza wenyewe.

Mmiliki wa bucha iliyozinduliwa, Othman Bhoke, alisema wazo la kuanzisha bucha hiyo alikuwa nalo miaka mingi, lakini hakujua namna anavyoweza kufanya ili apate vibali.

Alisema baada ya Rais Magufuli kutoa agizo hilo, aliamini ndoto yake imetimia na hivyo akaamua kuwa mtu wa kwanza kufungua bucha hilo na ameanza kujenga bucha nyingine katika Jiji la Arusha.

# Mahakama yatoa siku 14 Symbion kulipa wafanyakazi

**Na Christina Mwakangale**

DALALI wa Mahakama Kishe Auction Mart, ametoa tangazo la notisi ya siku 14 kwa kampuni ya kufua umeme Symbion Power Tanzania Limited, kulipa madai ya wafanyakazi kabla ya kunadi mali ya kampuni hizo.

Tangazo hilo lilibandikwa jana katika ofisi za kampuni hiyo zilizopo Ubungo, jijini Dar es Salaam, kufuatia Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi Tanzania, kuamuru kampuni hiyo kuwalipa wafanyakazi kiasi cha Sh. bilioni 12.

Martin Urio, msimamizi mwandamizi wa kufua umeme katika kampuni hiyo, akizungumza na waandishi wa habari jana, baada ya kutolewa tangazo hilo, alisema hatua hiyo ni ukombozi kwa wafanyakazi wote ambao wana madai ya takribani miezi 31.

"Wafanyakazi 43 tunaidai kampuni baada ya kushindwa kutulipa mshahara, tulifungua kesi yetu katika Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi, Agosti mwaka huu, tukidai takribani shilingi biloni 12," alisema Urio.

Siku 14 alizotoa 'court broker' ni fursa kwa mwajiri (Symbion) aidha kujipanga kuweka mambo sawa, kutulipa au yakatolewa maamuzi mengine na mahakama kabla ya siku hizo kutimia," aliongeza.

Mahakama hiyo ambayo ilimteua dalali huyo kushughulikia sula hilo, kampuni iliamriwa na mitambo yake kupigwa mnada kuwalipa wafanyakazi hao Sh. 12,249,890,439.

Kutokana na kampuni kusitisha shughuli zake, katika uamuzi wa shauri namba 60 la mwaka 2019, ulitolewa Novemba 13, mwaka huu na Nipashe kuona nakala hiyo, kwamba Naibu Msajili Warsha Ng'humbu, mawakili wa upande wa wadai na mjibu maombi hawakuwa na pingamizi lolote.

Pia, ilisomeka katika nakala hiyo, wafanyakazi wa kampuni hiyo walipwe haki zao. Ng'humbu alisema kuwa awali wafanyakazi hao waliungana na mwenzao Maganga Kadogosa, ambaye aliwasilisha kesi kudai kulipwa malimbikizo ya Sh. milioni 24 za mishahara yake.

Baada ya kushinda shauri hilo, wafanyakazi hao wakiwakilishwa na Alex Kisinga, waliungana kufungua shauri hilo wakitaka kulipwa malimbikizo ya mishahara yao.

"Shauri hili lilifunguliwa na Maganga Kadogosa, ambaye aliomba mahakama kutoa amri ya kulipwa kwa malimbikizo yake ya mishahara yaliyofikia Sh. 24,000,000.

"Kwa kuwa wafanyakazi hao walithibitishwa kama ilivyokuwa kwa Kadogosa kuwa walikuwa wafanyakazi wa mjibu maombi, mahakama iliwaunganisha katika shauri la madai wakiwakilishwa na Alex Kisiga," alisema naibu msajili katika uamuzi huo.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Sanaa, burudani chafu zinaliangamiza taifa

**NDANI** ya magari hasa mabasi ya mikoani anakopanda kila abiria kuanzia watoto wachanga hadi vikongwe, ni eneo la kuangamiza watoto na vijana wa taifa hili kimaadili.

Ni kwa vile kinachoonekana, kuimbwa na kutangazwa kwenye kazi za sanaa zinazowekwa kama burudani kwa abiria ni aibu na mmomonyoko wa maadili.

Ukweli usiopingika ni kwamba kinachojiri ni picha chafu za sinema, vichekesho na nyimbo za wasanii ambazo zinatia kichefuchefu, kukera na zaidi ni aibu.

Kinachoonyeshwa ni picha zisizo na maadili, mabinti kuvaa nguo zinazowaacha utupu, maneno ya matusi, kucheza kwa kujidhalilisha na matendo yaliyotarajiwa kufanywa sirini kutendeka hadharani.

Ni aibu na upungufu kwenye vyombo vya kusimamia maadili ya sanaa na usanii kushindwa kukomesha 'upotoshaji' huo ndani ya mabasi licha ya kwamba nao wakati mwingine ni wasafiri.

Tunapomaliza mwaka tunasema kuwa haipendezi. Tumeona na wengi watakuwa mashahidi wetu. Tumevumilia kwa muda mrefu ambao pia tunaamini imeonekana na serikali kwa kuwa wakati mwingine watendaji wake wanatumia usafiri huu.

Hatuna haja ya kupindisha ukweli kwa vile hii ni soni na kwa kiwango kikubwa kwani, ujumbe unatolewa kwa muda mrefu ndani ya kazi hizo za sanaa umepotosha na kujeruhi mioyo ya wengi.

Tunajua kuwa wapo wasafiri watoto, hawa tunajiuliza ni kwa kiasi gani wamepotoshwa na kuharibiwa dhamira zao hata kutumbukizwa kwenye shimo la wakosa maadili na burudani hizo?

Hatuishii hapo kwani tunafahamu kuwa ndani ya vyombo vya usafiri kuna viongozi mbalimbali, wakiwamo wa dini na watu waadilifu wamekerwa na picha hizo zenye mmomonyoko wa maadili.

Tunashauri kuwa tunapoanza mwaka mpya ni wakati wa kubadilika, vyombo vya kusimamia sanaa na maudhi yake viwajibike.

Kuna wakati kulikuwa na mtindo wa kuuza dawa za binadamu kwenye vyombo vya usafiri Mamlaka ya Chakula na Dawa (TMDA) ilifuatilia na kupiga marufuku.

Ni kwa kufuata utaratibu huo mamlaka za kufuatilia maadili kwenye sanaa na burudani ziamke ziwaige TMDA wakague vyombo hivyo kuanzia mabasi ya mikoani na vituo vya kurekodi muziki kuviona na kuwachukulia hatua kama si kuwaonya waandaaji (watunzi), waliorekodi na kusambaza kazi hizo zisizo na maadili.

Haipendezi kuruhusu muziki, vichekesho na sinema zenye maudhui machafu kusambaa na kuenea kila mahali bila kuchukua hatua na kuiacha tabia hiyo ikue na kuenea nchi nzima.

Inasikitisha kuwa usanii huo usio na tija umejaa kwenye 'YouTube' na unapatikana popote na ndicho kinachowavutia vijana na watoto wengi wanapokuwa na kutizama wakifurahia burudani inayowaangamiza.

Tunakumbusha kuwa mambo ya faraghani kuletwa ukumbini (hadharani) yamechangia watoto wetu shuleni au ndani ya jamii kupotoka kwa kuamini kuwa matendo yasio na maadili ni jambo zuri na la kupendeza kila wakati.

Yote hayo tunaona yamesababisha wasichana wetu kurubuniwa na kupata mimba udogoni, tunadhani kuwa yamesababisha kuongezeka matendo ya ovyo ndani ya jamii yetu hasa zinazowahusisha watoto.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Halima Ramadhani

# Waziri Lukuvi naomba unisikie kilio changu

**MIMI** Halima Ramadhani, mkazi wa Kongowe Vikuge Mkoa wa Pwani, nina mengi yanayoniliza moyoni na maishani, lakini linalonitesa na uzee wangu ni kuhusu kudhulumiwa shamba langu lenye ukubwa wa ekari takribani 13 liliko Vikuge.

Ndicho kilio changu kwako mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi. Najua umekutana na kusaidia wazee wengi kupata haki yao naomba nami unikumbuke.

Shamba langu nililinunua kwa Mzee Mkamba miaka 45 iliyopita nakumbuka na vielelezo ninavyo, ilikuwa Desemba 10, mwaka 1975 kwa gharama ya Shilingi 120,000.

Sikulinunua kwa siri na mashahidi wangu walikuwapo nao ni pamoja na Shehe Rashidi Mkendo pamoja na mjumbe wa Vikuge wa wakati huo, Hamba Sipoti.

Mume wangu wakati huo alikuwa mfanyakazi na alipata uhamisho kikazi akapelekwa Tanga, ikabidi tuondoke mkoani Pwani na kulilinda shamba kwa kulikabidhi kwa mwangalizi Iddi Udugu.

Ilitokea Iddi alinipigia simu na kunitaarifu kuwa shamba limeuzwa na mtoto wa Mzee Mkamba aliyeniuzia eneo hilo hapo awali, akimtaja kijana huyo kuwa ni Ally Mkamba, tulipata taarifa na mume wangu Juma Rajabu, tukachukua hatua.

Shamba liliuzwa na Ally Mkamba kwa Sheilla Simoni, lakini mimi Halima Ramadhani, ambaye ndiye mmiliki sikushirikishwa hivyo nilichukua hatua na kufika serikali za mitaa Vikuge kwa ajili ya shauri la shamba langu nikihoji na kutaka kupewa haki yangu.

Ally Mkamba, alikiri kuwa ametukosea na kuapa kuwa hataingilia tena shamba langu, lakini muda si mrefu kesi ilipelekwa mbele na nilipata wito wa kuitwa kwenye Baraza la Ardhi la Viguge kwenye shauri namba 11/2/2014 na nilishinda kesi hiyo chini ya Mwenyekiti wa Baraza, Juma Dugiza.

Niliendelea na shamba langu bila matatizo, lakini mwaka 2018 alijitokeza Sheilla Simoni na kunishtaki kuwa mvamizi wa shamba lake katika Baraza la Ardhi Kibaha.

Kuanzia mwaka 2018 mpaka leo sijasikilizwa wala shauri letu hilo halijasikilizwa na kutolewa maamuzi. Ndiyo maana nimeamua kufikisha malalamiko yangu kwako mheshimiwa Waziri wa Ardhi kwa barua hii, nikiomba kukufahamisha kuwa shauri hili halijasikilizwa pamoja na jitihada nyingi nilizofanya.

Mnamo Septemba 8, 2020 niliandika barua Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani kwa sanduku la barua (SLP 30080) nikimsihi na kumuomba anisaidie ili niweze kurudishiwa shamba langu.

Naona sasa ni muda mrefu na sijaweza kupata msaada naomba nifike tena mbele yako kukusihi unisaidie kwani, ninakosa wa kunisaidia na muda unakwenda bila mafanikio.

Mimi Halima Ramadhani ni mtu mzima tena mjane ninayetegemea ardhi yangu kumudu maisha haya. Nina wasiwasi sina wa kunisaidia mbali na serikali ambayo tunaiamini na kuitegemea kwa kuwa ndiyo mtetezi wetu sisi wanyonge ndiyo maana nakuomba Waziri unisaidie nipate haki yangu isitoshe kama nilivyosema mimi ni mjane.

Ninaomba unisikie kwa vile wale wenye dhamana ya kushughulikia suala hili hawajanisaidia na sasa tunaelekea mwaka wa tatu bila mafanikio, tumaini langu likibakia kwa serikali yetu ambayo wewe ni sehemu yake.

Nakushukuru kwa ushirikiano na ninaomba unisikie mimi mnyonge ambaye kimbilio langu ni serikali.

***Ni Halima Ramadhani na mawasiliano yangu ni haya: 0713 064727.***

## HABARI KITAIFA

### ASA Microfinance yapiga jeki shule vifaa

**Na Christina Mwakangale**

SHULE ya Sekondari Makumbusho, jijini Dar es Salaam, imepokea msaada wa vifaa vya shule ikiwamo mabegi ya kubebea madaftari 200, rimu 150 na kompyuta.

Mtendaji Mkuu wa ASA Microfinance Tanzania (Ltd), Muhammad Newaj, akikabidhi msaada huo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salam, alisema msaada kama huo hutolewa kwa wenye mahitaji maalum mara mbili kwa mwaka. Alisema taasisi hiyo inayojihusisha na utoaji mikopo kwa wajasiriamali wadogo, hutambua mchango wa elimu kuwa ni msingi wa maendeleo katika taifa na kwamba wanaunga mkono juhudi za serikali kuboresha sekta hiyo.

"Ukisoma itakuwa sehemu ya maendeleo katika taifa, kuendeleza maisha na ukimaliza masomo ukiomba ajira utapata kwa sababu umesoma. Kipaumbele katika umri wenu iwe ni kusoma, kusoma, kusoma. Taasisi yetu imeajiri Watanzania takribani 3,000, hata nyie mkimaliza mtapata fursa ya ajira kwetu," aliahidi Newaj.

### Lukuvi ataka gharama urasimishaji ardhi

**Na Munir Shemweta,** ARUSHA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amemwagiza Mkuu wa Chuo cha Ardhi Morogoro, Huruma Lugala, kukokotoa gharama halisi za uendeshaji urasimishaji ili aweze kupanga bei anayopaswa kulipa wananchi.

Alitoa agizo hilo jana jijini hapo alipokwenda Mtaa wa Muriet kukagua urasimishaji makazi unaofanywa na Chuo cha Ardhi Morogoro (ARIMO).

Alisema, wakati chuo hicho kikiendesha urasimishaji kwenye mitaa ya Mlimani, FFU, Msasani na Muriet, jijini Arusha ni vyema kikatumia kazi hiyo kama shamba darasa kwa kukokotoa gharama halisi ili kujua kiwango anachopaswa kuchangia mwananchi kwa kuwa kampuni binafsi haziwezi kuweka viwango halisi.

"Hii mitaa minne mliyopewa kurasimisha mfanye ukokotoaji wa kujua gharama halisi ili baada ya mwisho wa mwezi Januari mtakapokamilisha kazi hiyo nitangaze viwango halisi na mkisema gharama ni 50,000 nitatangaza kiwango hicho," alisema Lukuvi.

Kwa sasa kiwango cha mwisho kilichotangazwa na Waziri ambacho mwananchi anayerasimishiwa eneo lake ni 150,000.

Kwa mujibu wa Lukuvi, awali kila kampuni ilijiwekea kiwango chake na baada ya kuona viwango holela na kufikia hadi Sh. 400,000 nne aliamua kushusha hadi Sh. 150,000 na kubainisha kuwa hakuna kampuni iliyolalamikia ushushaji kiwango hicho na kusisitiza akipata kiwango halisi atajua gharama ya kumrasimishia mwananchi kwa nyumba moja.

# Naibu Waziri achukizwa miradi polisi kusuasua

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani, Khamis Hamza, amesema kuna miradi mingi ya Jeshi la Polisi Zanzibar inasuasua wakati imegharamiwa fedha nyingi.

Alisema miongoni mwa miradi hiyo ni ujenzi wa nyumba za polisi, Bububu Unguja unakaribia miaka mitano bila kukamilika.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumaliza kikao kati yake na uongozi wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Zanzibar.

Alisema atahakikisha anachukua hatua kwa wote waliozembea uzorotaji wa miradi hiyo ukiwamo pia ujenzi wa vituo vya polisi.

"Askari polisi wanafanya kazi katika vituo visivyorasmi wakati serikali imetoa fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa vituo na nyumba za askari," alisema.

Alisema kuna changamoto nyingi katika Jeshi la Polisi ikiwamo uzoroteshaji wa kesi za udhalilishaji, dawa za kulevya na rushwa kwa baadhi ya askari wa jeshi hilo.

Kadhalika, alisema baadhi ya askari wa jeshi hilo siyo waaminifu, wakituhumiwa na vitendo vya rushwa hasa kwa kesi za dawa za kulevya na udhalilishaji na baada ya kupokea rushwa hupoteza vielezo vya kesi hizo ili zisizonge mbele.

Alisema hivi sasa ni utawala mpya hivyo atatumia sheria na kanuni za nchi kuziondoa changamoto hizo na kuwachukulia hatua wanaohusika na vitendo hivyo.

Vilevile, alisema atazifanyia kazi changamoto zinazozikabili jeshi hilo ikiwamo uchakavu wa magari.

"Nafahamu kuwa askari wa Jeshi la Polisi mnafanyakazi katika mazingira magumu kulinda raia na mali zake pamoja na kusimamia amani na usalama wa nchi," alisema.

Naibu waziri huyo yupo Zanzibar kwa ajili ya kutembelea miradi mbalimbali ya Jeshi la Polisi ikiwa ni mara yake ya kwanza kuzungumza na watendaji wa jeshi hilo, Zanzibar baada ya kuteuliwa wadhifa huo.




Wajumbe wa Baraza la Tatu la Wafanyakazi la Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), lililofanyika katika ukumbi wa mikutano jijini Tanga, Desemba 18, wakiwa pamoja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe 22/12/2020

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMANNE** tarehe 22-12-2020 kampuni ya HAINAN INTERNATIONAL LTD itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **SINGIDA** kuelekea **DAR ES SALAAM**, gari hilo lenye namba za usajili:

**T 176 DFN / T 171 DFN.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 18.00 |
| Upana | - | mita | 3.00 |
| Kimo | - | mita | 5.00 |

3. Njia itakayotumika: **SINGIDA** hadi **DAR ES SALAAM** kupitia **MOROGORO**.

Gari itasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

MuCoBa Bank PLC

**TAARIFA YA KUAIRISHWA KWA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA MOJA (21) WA WANAHISA WA BENKI YA MUCOBA**

Taarifa inatolewa kwa wanahisa kwamba, Mkutano Mkuu wa ishirini na moja wa Wanahisa ulio takiwa kufanyika siku ya Jumatano tarehe 23 mwezi wa Disemba 2020 katika ukumbi wa MAM –uliopo Mafinga Mjini umeairishwa mpaka hapo tutakapo watangazia tena.

Samahani kwa usumbufu uliojitokeza.

**KWA AGIZO LA BODI YA WAKURUGENZI**
**PHILIP RAYMOND PHANUEL**
**KATIBU - BODI YA WAKURUGENZI**

# Jaji Mkuu: Mawakili zingatieni Katiba

**Na Sabato Kasika**

JAJI Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma, amewataka mawakili kutimiza wajibu wao kwa kuzingatia Katiba, sheria za nchi na mahakama bila kupotosha uamuzi unaotolewa na mahakama.

Prof. Ibrahim alisema hayo jijini Dar es Salaam jana, kwenye sherehe ya kuwakubali na kuwapokea mawakili wapya 166 na kufafanua kuwa kumekuwapo na malalamiko mengi kuhusu utendaji wa mawakili.

"Nendeni mkatimize wajibu wenu kwa kuzingatia Katiba, sheria za nchi na mahakama kwa kuwa wapo mawakili wachache wakitumia lugha zisizofaa, kupotosha maamuzi ya mahakama na wanalalamikiwa," Prof. Juma alisema.

Jaji Mkuu alisema, wapo pia baadhi ya mawakili wenye sifa za ujanja ujanja na wateja wenye sifa hizo, ambao huchelewesha kesi na kusababisha migogoro isiyoisha katika jamii.

"Wapo mawakili wengine husumbua wateja na wakati mwingine kuwakatia mawasiliano, hasa wanapoona fedha wateja wao ni ndogo, lakini ninaamini kwamba ninyi hamtakuwa wa aina hiyo," alisema.

Naye Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk. Evaristo Longopa, alisema mawakili ni maofisa wa mahakama na kwamba chini ya sheria ya mawakili, wao ni sehemu kubwa ya kuhakikisha mahakama zinafikia uamuzi wa haki.

"Mawakili hawatakiwi kuwa watoro, kudanganya mahakama kwa mbinu mbalimbali za uongo kwa ajili ya kutaka ushindi, kwa kuwa idadi ya wakiukaji wa maadili inakuwa siku hadi siku," alisema Dk. Longopa.

Alisema, kazi ya uwakili ni muhimu katika ustawi wa nchi na kuwataka waache kutoa lugha mbaya kwa mawakili wenzao na kufanya kazi hiyo kwa uaminifu na pia kuongeza ujuzi kadri inavyoezekana.

Dk. Longopa aliwataka mawakili hao kuacha njia ya mkato katika utendaji wao wanapohudumia wateja hata kama wanatoa msaada wa kisheria wanalipwa na jambo la msingi ni kuzingatia maadili ya kazi.

Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Lugemeleza Nshala, aliwataka mawakili hao kutambua kuwa kazi hiyo ni ya heshima na waishi kulingana na jinsi inavyoheshimika.

"Mawakili wapya ni vyema muishi kwa kuzingatia hilo, kwamba kazi hii ndiyo maisha yenu na inaheshima kubwa katika jamii, hivyo muifanye inavyotakiwa na tena kwa uaminifu mkubwa," alisema Nshala.




Mshindi wa tatu wa promosheni ya Vodacom Shangwe Shangwena mkazi wa Kigamboni, Peter John, akifungua mlango wa gari jipya aina ya Renault KWID baada ya kukabidhiwa jijini Dar es Salaam juzi. Anayeshuhudia (kushoto) ni Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Sarah Msafiri. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC ataka taarifa ujenzi chuo VETA

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Marwa Rubirya, amemwagiza Mkurugenzi wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) Nyanda za Juu Kusini, kuandaa taarifa itakayoonyesha lini ujenzi wa chuo cha VETA Shaurimoyo, wilayani Ludewa utaanza baada ya kusimama kwa muda mrefu.

Alitoa agizo hilo juzi baada ya kufanya ziara katika eneo la ujenzi wa chuo hicho, kilichopo Kijiji cha Shaurimoyo, Kata ya Lugalawa.

Alisema ifikapo mwisho wa mwezi huu, anahitaji kupatiwa taarifa ambayo itaonyesha hatua zilizopangwa kuanza nazo katika ujenzi wa chuo hicho.

Rubirya alisema chuo hicho kinajengwa kimkakati na siyo kwa bahati mbaya kwa kuwa kinahitajika na wakazi wa Mkoa wa Njombe na siyo Ludewa pekee yake.

"Nilikuwa nawaambia kwenye baraza, huwezi kuzungumzia Njombe bila ya Liganga na Mchuchuma, hivyo chuo hiki hakikuamriwa kijengwe hapa kwa bahati mbaya bali kinajengwa kimkakati," alisema Mhandisi Rubirya.

Aliwahakikishia wakazi wa kijiji hicho kuwa mahitaji ya chuo hicho bado yapo pale pale na chuo hicho kitajengwa eneo lililokusudiwa kwa sababu wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne kijijini hapo waweze kupata mafunzo.

Awali, akitoa maelezo ya mwenendo wa ujenzi wa chuo hicho, mwakilishi wa Mkurugenzi wa VETA, Benitho Kigava, alisema mradi huo wa ujenzi wa chuo hicho ulianza Januari, 2017 na ulipaswa kukamilika katika kipindi cha miezi minane.

Alisema mradi huo ulikuwa ukijumuisha majengo ya karakana, madarasa, ofisi za utawala, mabweni, nyumba za watumishi, vyoo na miundombinu ya nje ikiwamo barabara.

Alisema katika mradi huo kiasi cha gharama ambacho kilipaswa kutumika katika ujenzi wa chuo hicho ni zaidi ya Shilingi bilioni tisa.

Alisema mkandarasi alikabidhiwa mradi huo Desemba mwaka 2016 na alianza kazi Januari 2017, alipaswa kumaliza mradi huo kwa muda wa miezi minane.

"Ninachoweza kusema huu mradi mtu ambaye hakuutendea haki wa kwanza ni mshauri wa mkandarasi, kwani ndiye aliyeshauri ili majengo yajengwe."

Mbunge wa Ludewa, Joseph Kamonga, alisema akiwa Ofisa Ardhi wa Wilaya ya Ludewa, alishiriki katika kuandaa hati ya eneo hilo ambalo lilitolewa na wananchi kwa ajili ya ujenzi wa chuo hicho.

Alisema wananchi walitambua umuhimu wa kujengwa kwa chuo hicho, lakini cha kushangaza jambo hilo limechukua muda mrefu zaidi ya miaka 10.

"Baadhi ya wananchi walimweleza mkuu wa mkoa kwamba kama chuo hiki hakipo tena basi turudishiwe mashamba yetu ili tuendelee kulima."

Nao baadhi ya wakazi wa kijiji hicho cha Shaurimoyo, akiwamo Nicholaus Kayombo, alisema wanakitegemea chuo hicho, lakini cha kushangaza hakuna utekelezaji wowote unaoendelea.

## NHC yatangaza kiama wadaiwa sugu

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC), limewataka wapangaji wake wenye malimbikizo ya kodi kulipa madeni hayo kabla ya muda uliowekwa, ili kuepuka usumbufu wa kupigwa mnada mali zao.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na NHC, zimetolewa siku 30 kwa wapangaji wanaodaiwa kodi na malimbikizo kufika katika ofisi za shirika zilizo karibu yao ili kulipa kodi wanazo daiwa.

Shirika limewashauri wapangaji wote kutumia fursa hiyo, kulipa madeni yao kabla ya muda uliowekwa kupita.

Pia shirika liliwashukuru wapangaji wote waliotekeleza maagizo waliyopatiwa baada ya kupewa siku 14 za kulipa kodi na malimbikizo.

## Kwaya 40 zashukuru taifa kuepushwa corona

**Na Rose Jacob,** MWANZA

ZAIDI ya kwaya 40 za madhehebu ya Kikiristo mkoani Mwanza, zimefanya tamasha la kumshukuru Mungu kwa kuliepusha taifa na ugonjwa wa corona pamoja na kuivusha nchi salama kwenye uchaguzi mkuu wa Oktoba 28.

Tamasha hilo liliandaliwa na umoja wa makanisa mkoani Mwanza kwa kushirikiana na ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza kupitia kitengo cha utamaduni.

Akizungumza katika tamasha hilo kwa niaba ya Baba Askofu, Lenatus Mkwande, Padri Bagusu Mayanga, alisema Watanzania wanajukumu kubwa la kuingia katika maombi ya kumshukuru Mungu kwa kumrudishia sifa.

Kwa upande wake, Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Makanisa mkoani Mwanza, Askofu Yohana Hulilo wa Kanisa la City Worship Center alisema, maombi ya wasio haki ni kelele hivyo viongozi wa nchi wanaposimamia kwa haki, lazima Mungu atasikia maombi yao.

Aliwataka Watanzania kuendelea kumpatia ushirikiano Rais John Magufuli ili aendelee kuleta maendeleo yaliyo ndani ya haki badala ya kumkatisha tamaa.

## CCM yaagiza utatuzi migogoro wafugaji/wakulima

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Shinyanga kimewataka madiwani wa Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama, kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji katika maeneo yao.

Katibu wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Donald Magesa, aliyasema hayo jana, wakati akizungumza na madiwani wa halmashauri hiyo.

Alisema kila diwani anatakiwa kuhakikisha kwenye eneo lake hakuna migogoro ya wakulima na wafugaji.

Aliongeza kuwa kila diwani anatakiwa kushawishi ili kutengwa maeneo maalumu kwa ajili ya kilimo na mifugo ili kutekeleza majukumu yao bila kuingilia na kuibua migogoro.

## Simiyu yatangaza vita wanaosababisha kashfa

**Ndalike Sonda,** SIMIYU

SERIKALI mkoani Simiyu imetangaza vita dhidi ya watumishi wa umma wanaosababisha mkoa huo kuingia katika kashfa ya wizi wa mitihani ya taifa.

Katibu Tawala wa Mkoa huo, Mariam Mmbaga, alisema hayo wakati akitangaza wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mkoani humo, Januari mwaka 2021.

Mmbaga aliagiza hatua kali zichukuliwe kwa wanaotajwa kuhusika na udanganyifu huo katika mtihani wa taifa wa darasa la saba na Mkoa wa Simiyu kufutiwa matokeo kwa baadhi ya shule zake.

## Wafanyabiashara wanawake waaswa mikopo

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

WAFANYABIASHARA wanawake wilayani Kahama, wametakiwa kuachana na mikopo ya mitaani kutokana na kutapeliwa na kuwasababishia umaskini.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Annamringi Macha, alitoa tahadhari hiyo alipokutana na wanawake katika kongamano la wanawake wafanyabiashara lililoandaliwa na Benki ya CRDB na kuhudhuriwa na wanawake zaidi ya 250.

"Ukopeshwaji wa fedha kwa wale matapeli hutoa riba ya asilimia 40 hadi 50 mtu anakopa shilingi millioni moja, lakini kurejesha anaaambiwa atoe kiasi cha shilingi millioni 1.5 na mikataba wanayosainishana inaonyesha wameuziana mtiririko wake wote ni utapeli hilo nimeshuhudia kesi zimenifikia ofisini kwangu," alisema Macha.

# Lukuvi aagiza ukaguzi mashamba makubwa

**Na Mary Mosha,** SAME

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amawaagiza makamishna wa ardhi kwa ngazi za mkoa nchini, kufanya ukaguzi kwenye mashamba makubwa kukagua uendeshaji, ulipaji kodi na utoaji wa ajira kwa vijana.

Pia, ametoa mwaka mmoja kwa mwekezaji wa shamba la mkonge la Ndungu, linalomilikiwa na Kampuni ya L.M Investiment Ltd kupanda mkonge kwenye ekari 2,000 alizonazo.

Alitoa agizo hilo juzi wilayani Same, mkoani Kilimanjaro, wakati akikabidhi heka 300 kwa vijiji vya Ndungu, Mpirani na Msufini.

**Wataalamu hakikisheni kazi hiyo inaanza mara moja, hii itasaidia kutokomeza wawekezaji wasio na tija katika taifa.**

Alisema, ukaguzi huo utasaidia kuwabaini wawekezaji wasio na tija katika jamii.

"Wataalamu hakikisheni kazi hiyo inaanza mara moja, hii itasaidia kutokomeza wawekezaji wasio na tija katika taifa," alisema.

Aliwataka wananchi wa Kata ya Ndungu kupata hati kwa kuwa tayari eneo hilo limetangazwa kuwa ni la mpango mji.

"Wananchi maeneo haya hampewi bure ila mtachangia gharama za utafutwaji wa hati na kuendelea kulipa kodi zenu kama kawaida," alisema Lukuvi.

Baadhi ya wananchi akiwamo Mohamed Iddy, alishukuru serikali kwa uamuzi huo na kuiomba iangalie utoaji pembejeo kwa vijana ili waweze kujikita katika kilimo cha umwagiliaji.

Alisema miongoni tatizo lililoikumba jamii ni pamoja na ukosefu wa ajira na kwamba ufufuaji wa maeneo ya mashamba utasaidia kuwavutia vijana katika kilimo.

Awali, akimkaribisha waziri, Mkuu wa Wilaya hiyo, Rosemary Sinyamule, alisema wataalamu wake tayari wameshapima maeneo yote na hekari hizo zitakabidhiwa kwa wananchi mambo madogo yatakapokamilika.

"Maeneo yote yameshapimwa na yatakabidhiwa kwa wananchi kama ilivyoelekezwa, jukumu la wananchi ni kuyaendeleza maeneo hayo ili yaweze kuleta tija kwa jamii na taifa kwa ujumla," alisema.




Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija (watatu kushoto), akipokea tuzo ya heshima kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, iliyotolewa kwa Rais Dk. John Magufuli, kutoka kwa Mkurugenzi wa Karibu Dodoma Festival (KDF), Simon Mwapagata 'Rado', wakati wa hafla ya utoaji tuzo na shukrani iliyoandaliwa na wasanii, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wakutubi kupewa kipaumbele ajira

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, amesema wizara hiyo itajitahidi kutoa kipaumbele cha ajira za wakutubi katika shule za msingi na sekondari, ili vyumba vilivyojengwa kama maktaba vitumike kwa kuhudumiwa na wataalamu wa fani husika.

Silinde aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mahafali ya 26 ya Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi wa Nyaraka, Bagamoyo mkoani Pwani.

Alisema serikali inasisitiza kuondoa ujinga na kumfanya kila mtoto kujua kusoma na kuandika na kwamba wakutubi wana mchango mkubwa kuamsha ari ya kupenda kusoma.

"Nitahakikisha angalau kila maktaba ya shule iwe na mkutubi, ili vitabu vinavyopelekwa shuleni visiwekwe stoo na kuchakaa kwa vumbi, naahidi pia wizara yangu itaendelea kushirikiana na Wizara ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kuhakikisha wahitimu wa chuo hiki wanapata ajira ya moja kwa moja kama ilivyo kwa walimu na madaktari," alisema.

Alisema TAMISEMI itawaagiza wakurugenzi wote kuhakikisha kila shule mwalimu mmoja anahudhuria mafunzo ya ukutubi na uhifadhi wa nyaraka katika chuo hicho.

Alisema shule nyingi zina vyumba vya maktaba ambavyo vinatumika kuhifadhi vitabu na kwamba hakuna wakutubi wa kutosha kuhudumia maktaba hizo.

Mkuu wa chuo hicho, Victoria Kessy, alisema udahili wa kuanzia mwaka 2017 hadi 2020 unaonyesha kupungua kwa idadi ya wanachuo ikilinganishwa na 2010-2015 idadi ya wanachuo ilifikia 1,000 na miongoni mwa sababu kuwa ni pamoja na ufinyu wa ajira.

Alisema takwimu nchini zinaonyesha kuwa ni shule chache za msingi na sekondari zilizo na maktaba na kuajiri wakutubi wenye sifa.

Victoria alisema baadhi ya vikwazo vinavyokikabili chuo hicho kuwa ni pamoja na uchakavu wa vyombo vya usafiri, ukosefu wa huduma za kuaminika ya mitandao, upungufu wa kumbi za mihadhara na vyumba vya madarasa.

Katika risala ya wahitimu iliyosomwa na Fredrick Kapinga, ilieleza kuwa tatizo la ajira ni chanzo cha kukatisha tamaa wengine waliokuwa na lengo la kusomea fani hiyo.

# Wananchi watakiwa kuwafichua wahalifu

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

WATENDAJI wa kata na vijiji mkoani Mtwara kwa kushirikiana na wananchi wa pembezoni mwa nchi ya Msumbiji wametakiwa kuwafichua wahalifu wanaoishi nao kwenye nyumba zao.

Wito huo ulitolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, alipofanya ziara kwenye baadhi ya kata zilizo pembezoni mwa nchi ya Msumbiji, zikiwamo za Mahurunga, Tangazo na Dihimba Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, ziara ambayo pia ililenga kutoa elimu kwa wakulima ya kuongeza uzalishaji bora mazao ya kilimo.

**Tabia hizo zinahatarisha amani na utulivu kwenye kata hizo na wananchi kushindwa kuishi kwa amani na utulivu.**

Byakanwa aliwataka wananchi wa maeneo hayo kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo wanayoishi usiku na mchana ili kudumisha amani na utulivu katika vijiji vyao.

Alisema serikali mkoani humo imebaini kuwapo baadhi ya wananchi kata za Mahurunga, Tangazo na Dihimba wenye tabia ya kuwahifadhi wahalifu kwenye nyumba zao ili kuwasaidia kufanya uhalifu kwa kupewa kiasi kidogo cha fedha.

Alisema tabia hizo zinahatarisha amani na utulivu kwenye kata hizo na wananchi kushindwa kuishi kwa amani na utulivu.

Aliwaagiza watendaji kata na vijiji kusimamia amani na usalama kwenye maeneo yao ili kuendeleza utulivu uliopo.

Byakanwa alisema watendaji hao wanapaswa kuanza kuorodhesha vijana wote ambao hawajulikani walipo na wanafanya nini huko waliko ili serikali mkoani humo iwatambue.

"Taarifa tulizonazo Wanamtwara wote mnaokaa kwenye mipaka hii mnatabia ya kuficha wahalifu kwenye majumba yenu kwanini hamtoi taarifa za kuwapo kwa wahalifu hao sasa wale wenye watoto ambao hawajulikani waliko na wanafanya nini nataka watendaji mnipatie majina yao," alisema Byakanwa.

Alisema kwa upande wa serikali mkoani humo vyombo vya ulinzi na usalama vimeimarisha ulinzi na usalama, hali imekuwa shwari na wananchi wanaendelea kuishi kwa amani na utulivu.

Alisema wananchi wakishirikiana vyema na serikali kwa kutoa taarifa itakuwa rahisi kuwabaini vijana wanaohatarisha amani na usalama kwenye maeneo hayo.



Meneja wa NMB Kanda ya Magharibi, Sospeter Magesse (wa pili kushoto), akikabidhi sehemu ya mabati 400 yenye thamani ya Sh. milioni 10 kwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako (katikati), kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa madarasa ya Shule ya Sekondari Ruhita na Kidiama wilayani Kasulu, mkoani kigoma. Makabidhiano hayo, yalifanyika katika Shule ya Sekondari Ruhita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkuranga kufanya msako maduka yanayouza dawa feki

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, inatarajia kuanza msako katika vitongoji vyote ili kupambana na maduka feki yanayouza dawa za binadamu bila ya kufuata taratibu za kisheria za kutoa huduma hizo kwa jamii.

Hayo yalisemwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya hiyo, Stephen Mbwambo, katika sherehe za maadhimisho ya siku ya wamiliki wa maduka ya dawa muhimu Mkoa wa Pwani.

"Tunatarajia kuanza msako mkali katika vijiji vyote kwa kukagua maduka feki ambayo yanauza dawa za binadamu, bila kufuata sheria za uuzaji dawa hizo," alisema.

Ofisa Tarafa wa Mkuranga, Clement Muya, aliipongeza Asasi ya PWAMAO, kwa kusaidiana na serikali kufuatilia ubora wa huduma zinazotolewa na maduka ya dawa muhimu, huku akiwahakikishia kuwa nao bega kwa bega hatimaye wananchi wawe na afya nzuri.

Mwenyekiti wa asasi ya wamiliki wenye maduka ya dawa muhimu Mkoa wa Pwani, Said Kipipa, alisema kuandaa kongamano hilo ni kulenga kuhimiza wamiliki wa maduka kufuata kanuni na sheria za utoaji huduma ambazo zinagusa kwa karibu maisha ya watu.

Katika sherehe hizo, mdau wa maendeleo na mfanyabiashara wa Mkuranga, Ahmed Salum, alikabidhi baiskeli 10 kwa ajili ya watu wenye ulemavu kupitia makundi yote, fimbo tatu ambazo zinasaidia kuwaongoza wasioona na magongo saba kwa wenye ulemavu wa viungo.

Awali, Ahmed aliwahi kusaidia magodoro 70 kwa ajili ya maandalizi ya kuwapokea wagonjwa wa corona Mkuranga, pia alichangia Sh.milioni mbili kwa ununuzi wa madawati wilayani hapo na viroba 300 kwa ya watoto wenye uhitaji Siku ya Mtoto wa Afrika.

## DC ashauri wahitimu Jeshi la Akiba waajiriwe

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

MKUU wa Wilaya ya Mtwara, Dunstan Kyobya, amezishauri taasisi za serikali na zisizo za kiserikali kuona umuhimu wa kutoa ajira kwa vijana waliohitimu mafunzo ya Jeshi la Akiba mkoani humo ili kupunguza tatizo la ajira.

Ushauri huo aliutoa jana mkoani hapa wakati alipokuwa akifunga mafunzo ya jeshi hilo na jumla ya vijana 137 walihitimu mafunzo hayo.

Alisema ili kakabiliana na tatizo la ajira kwa vijana, inapaswa taasisi za serikali na zisizo za kiserikali kuona umuhimu wa kutumia fursa ya kuajiri vijana wenye ujuzi ili waweze kutumia ujuzi wao.

Kyobya alisema wapo vijana wengi wenye ujuzi na uwezo mkubwa wa kufanya kazi walizopatia mafunzo na kama watapatiwa ajira kwenye taasisi hizo watachangia sehemu ya maendeleo ya taifa kwa nchi yao.

Alisema kupitia mafunzo hayo, vijana zaidi ya 137 wamehitimu mkoani Mtwara na tayari wana uwezo mkubwa wa kutumia vyema mafunzo waliyoyapata.

## Equity kuanzisha bima wakulima

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI inayotoa huduma za kifedha, Equity Bank Limited, inatarajia kuanzisha huduma za bima za kibenki, ikiwamo wakulima kufidiwa wanapopata majanga kabla ya mavuno.

Kupitia huduma hiyo, Equity Bank Limited inatarajia kutoa huduma za bima ya mazao ambayo wakulima wataweza kwenda kwenye benki hiyo na kupata huduma za kulinda mazao. Benki hiyo pia jana ilizindua utambuzi mpya unaoendana na safari ya mabadiliko inayoendelea ndani ya kampuni.

Utambuzi huo mpya unalenga kuiweka kampuni katika njia ya ukuaji endelevu na utoaji huduma bora, zinazoendana na mabadiliko yanaoendelea katika mazingira ya sekta ya fedha.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa huduma hiyo mpya, Mkurugenzi Mtendaji wa Equity Bank Limited, Robert Kiboti, alisema huduma hiyo itawalenga zaidi wakulima.

Akizungumza kuhusu uzinduzi wa nembo mpya, Kiboti alisema mwonekano huo unaambatana na ahadi ya usimamizi imara wa uhusiano, uwezeshaji wa wateja binafsi na biashara.

"Tutaendelea kubuni huduma bora kwa lengo la kupanua upatikanaji wa huduma jumuishi za kifedha nchini kote...Tutaimarisha upatikanaji wa huduma za kibenki kwa njia ya simu za kiganjani na kupeleka huduma zetu mpaka maili ya mwisho kupitia Equity Wakala," alisema Kiboiti.

Nipashe
# TESA
Jumanne Desemba 22, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

**Waja na ujasiriamali kuwaokoa mabinti na uhalifu wa kingono**



Ukurasa 13

TAS inavyopambana na saratani ya ngozi, yasambaza mashine kutoa tiba



Ukurasa 14

**Dk. Hellen Kijo - Bisimba atoa ushuhuda unaochoma, kuonya na kutaka kazi zaidi**

TEKNOLOJIA

NA SABATO KASIKA

# TEHAMA MAHAKAMANI

- Kesi kuendeshwa bila majalada
- Si lazima kuhudhuria kortini

NI ukweli usiopingika kwamba dunia imebadilika, hivyo mambo mengi yanafanyika kulingana na sayansi na teknolojia na ubunifu zaidi unaosukumwa na matumizi ya kompyuta au simu za mkononi zikiwa injini ya kufanikisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Ni zama mpya ya kimawasiliano na kufanyakazi kumerahisika na kuimarika kutokana na kukua kwa teknolojia zenye miundombinu isiyohitaji kuunganisha nyaya marufu kama 'wireless', na mawimbi ya mawasiliano yakitua kwenye simu na kompyuta kwa njia ya masafa ya Wi-Fi (wai-fai).

Matumizi ya teknolojia hiyo yanasambaa kwa kasi na safari hii sekta ya sheria, inatangaza kutumia TEHAMA na kufanyakazi kielektroniki katika kutoa haki.

Mazoea ya kuhangaika na mafaili mahakamani, wakati mwingine kesi kuahirishwa kutokana na madai ya faili kupotea, mashahidi, washtakiwa au walalamikaji kuchelewa sasa yanakwisha baada ya TEHAMA kupewa nafasi.

Ni machweo mapya kwa mahakama za Tanzania ambazo sasa zinajikita kwenye matumizi ya TEHAMA na kuwa mahakama isiyotumia karatasi, na inaanza na Mahakama ya Wilaya Kigamboni kama eneo la majaribio.

Anasema Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dk. Eliezer Feleshi, kwa niaba ya Jaji Mkuu Profesa Mohamed Juma.



Jaji Kiongozi, Eliezer Feleshi.

Anaongeza kuwa mahakama inategemea kupanua wigo kwa kuzifikia mahakama za wilaya zenye majengo mapya na ya kisasa zikiwamo za Kibaha, Chato na Ilemela.

"Kwa kuwa hatima yetu sote ni moja, mahakama inapoendelea kutumia TEHAMA katika kutoa huduma za ufunguaji, usikilizwaji na manejimenti ya mashauri wadau katika sekta ya utoaji haki lazima tuwe pamoja na kwa kasi moja," anasema Feleshi.

Anasema, dunia kwa kiasi kikubwa inaendeshwa na matumizi ya TEHAMA na kwamba nchi nyingi ambazo zimepata mabadiliko makubwa ya kiuchumi kutokana na matumizi ya mfumo huo, hivyo hata mahakama nazo hazina budi kuwa sehemu ya sayansi na teknolojia katika kufanikisha jukumu la kutoa haki na haki kuonekana ikitendeka.

Anasema, uharakishaji wa utoaji haki hauwezi kutenganishwa na matumizi ya bora ya TEHAMA na kwamba kwa msingi huo, anaamini mfumo huo ni nyenzo muhimu katika kuwezesha utoaji haki kwa wakati na kusogeza huduma za mahakama karibu zaidi na wananchi.

"Hivyo mahakama na wadau wake hawawezi kubaki nyuma kwani mapinduzi ya TEHAMA yameshakubalika na dunia iliyoshindani kuwa ni muhimu katika utoaji huduma za haki," anasema Jaji Kiongozi.

Jaji Kiongozi anapozungumza kwa niaba ya Jaji Mkuu wa Tanzania, wakati akifungua kikao cha kamati ya kusukuma mashauri ya madai, kilichokutana jijini Dar es Salaam, anasema serikali imewekeza katika eneo hilo.

### UWEKEZAJI TEHAMA

Feleshi anasema, mahakama imefanya uwekezaji mkubwa katika TEHAMA, ambayo ni lazima pia uwabebe wadau wa sekta ya sheria, ili wafaidike katika kutumia huduma nyingine za mahakama, ikiwamo usimamizi wa shughuli za mawakili, madalali na wapeleka nyaraka na shughuli nyingine za kiutawala kwa ujumla.

"Mapinduzi katika matumizi ya TEHAMA yanawezekana, kwani uwekezaji umefanywa katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na pia sera na sheria tayari vipo ili kufanikisha matumizi ya mfumo huo katika utoaji wa huduma za mahakama," anasema na kuongeza kuwa mwelekeo wa sasa katika matumizi ya TEHAMA ni kuwa mahakama isiyotumia karatasi.

Anasema faida zake ni uharakishaji wa utoaji haki ambao hauwezi kutengwa na matumizi ya bora ya teknolojia na kwamba kwa msingi huo, anaamini kuwa matumizi bora ya mfumo huo ni nyenzo muhimu katika kuwezesha utoaji haki kwa wakati na kusogeza huduma za mahakama karibu zaidi na wananchi.

### MANUFAA YA TEHAMA

Inaelezwa kuwa mfumo huo una manufaa mengi, kuanzia kutunza kumbukumbu, kama njia ya kupunguza mrundikano wa karatasi na kuwezesha ofisi kuwa na kompyuta chache zenye uwezo wa kutunza kumbukumbu.

Jaji Kiongozi, Dk. Feleshi, anataja mengine kuwa ni kupata taarifa kwa urahisi juu ya kesi kama imekwisha au inaendelea na pia unarahisisha kupokea ushahidi ikiwamo utoaji wa ushahidi kwa njia ya video.

"Mfumo huo pia unasaidia kuwapo wa usalama wa nyaraka mbalimbali hata wakati yanapotokea majanga ya moto, kupotea au uharibifu wa baadhi ya taarifa na kwamba kutumia TEHAMA, mahakama zinaweza kuokoa na kuhifadhi nyaraka muhimu salama," anasema Dk. Feleshi.

Anaeleza kuwa si manufaa hayo tu bali mengine ni kukoa muda na kupunguza urasimu na kumwezesha mwananchi anayehitaji nyaraka, zikiwamo nakala za hukumu kuzipata kwa wakati anapotaka kujua tarehe ya kesi.

"Vilevile mwananchi anaweza kupata haraka baada ya kuingia katika mfumo hata akiwa nyumbani, kuliko kutumia nauli na muda mwingi kufika mahakamani kuulizia," anasema.

Anasema, teknolojia hiyo italinda usalama wa mashahidi kwa vile inamwezesha shahidi kutoa ushahidi kwa njia video pasipo kufika au kuwapo mahakamani.

INAENDELEA UK.13

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Waja na ujasiriamali kuwaokoa mabinti na uhalifu wa kingono

WASICHANA wenye miaka kati ya 19 hadi 24 ambao walishindwa kuendelea na masomo na kubaki mitaani, kutokana na sababu mbalimbali, baadhi wanakabiliwa na changamoto za umaskini unaodaiwa kuwalazimisha kujihusisha na ngono, ili kujikimu.

Shinyanga inaelezwa kuwa ni miongoni mwa mikoa inayokabiliwa na tatizo la wasichana kujihusisha na ngono, kutokana na kukosa uelekeo wa maisha, ili mradi kupata fedha.

Wadau wa kutetea ustawi wa mabinti likiwamo Shirika la Kijamii la Restless Development linasema kinachoweza kuwanusuru ni pamoja na kuwapa mafunzo ya makuzi, haki, afya ya uzazi na ujasiriamali.

Kupitia mradi wa "vijana tunaweza" unatoa mafunzo kwa wasichana wenye umri wa kuanzia miaka 19 hadi 24 wanaoishi mitaani na wasioendelea na masomo, wasichana wanatarajiwa kunufaika na fursa hiyo, kwa mujibu wa mratibu wa mradi huo, John Eddy.

Anasema wanatoa mafunzo kwa wasichana 30 wanaoishi Manispaa ya Shinyanga kutoka kata za Old Shinyanga, Ndala na Ndembezi, ili wawe mabalozi kwa wenzao na kisha kuanzisha vikundi vya ujasiriamali.

Anaamini wakipewa elimu ya ujasiriamali na kuunganishwa kwenye vikundi na kupewa mikopo ya halmashauri ambayo ni asilimia 10, kwa mgawanyo wa asilimia 4.0 kwa vijana, mbili kwa wenye ulemavu na nne nyingine kwa wanawake, itawasaidia kupata fedha za kuendesha maisha yao na kuacha mambo yanayowadhalilisha.

"Lengo ni kupunguza visababishi vya wasichana walioko kwenye mazingira magumu mitaani kujiingiza kwenye makundi mabaya ambayo yatawasababishia kupata maambukizi ya VVU, mimba na kujiingiza kwenye uhalifu na kukosa mustakabali wa maisha yao," anasema Eddy.

"Tunaamini wasichana hawa wakitoka hapa watakwenda kuanzisha vikundi vya ujasiriamali, ili wapate fedha za kuendeshea maisha yao sababu tayari wameshapewa elimu hiyo na wataalamu kutoka halmashauri. Na watakuwa mabalozi bora kwa wenzao na kuwatoa kweye makundi ya kushiriki ngono," anaongeza mratibu huyo.

Miriam Mgaya ni mwenyekiti wa kikundi hicho cha wasichana 30, anasema wenzao wanaoishi mitaani hawana kazi na wanakumbana na changamoto nyingi za kimaisha hasa kukosa kipato na kulazimika kuingia kwenye




Mkurugenzi wa Halmashauri ya Shinyanga Geoffrey Mwangulumbi, akizungumza na baadhi ya wasichana 30 (pichani chini), ambao wamepewa elimu ya makuzi, afya ya uzazi na ujasiriamali na Restless Development. **PICHA: MARCO MADUHU.**

biashara ya kujiuza.

Anasema msichana mwenye miaka kuanzia 18 ana mahitaji mengi, hivyo wanapokosa fursa za kuwezeshwa ni lazima wapate vishawishi vya kujiingiza kwenye uhalifu au ngono wakiamini kuwa ndiyo njia rahisi ya kupata fedha haraka bila ya kujali madhara ya baadaye.

"Tunaiomba serikali, maofisa maendeleo ya jamii na wadau wengine kutoa elimu ya ujasiriamali kwa wasichana hawa pamoja na kuwapatia mikopo kuendeleza biashara na kupata fedha ili kuwaepusha na mambo yanayohatarisha maisha yao hasa maradhi," anasema Mgaya.

"Sisi 30 tuliopata mafunzo ya ujasiriamali na elimu ya afya ya uzazi kupitia Shirika la Restless Development, maisha yetu yameshabadilika na tayari tumeshaunda vikundi vya ujasiriamali, katiba yetu na sasa tunafanya taratibu nyingine ili tupate mkopo wa halmashauri," anaongeza mwenyekiti.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga Geoffrey Mwangulumbi, anaipongeza Restless Development, kwa kuwaibua wasichana hao na kuwajengea uwezo wa kujitambua na kufanya shughuli mbalimbali ambazo zitawaingizia kipato ili wajikwamue kimaisha.

Anasema Shinyanga kuna fursa nyingi za kibiashara ambazo vijana wanaweza kuzitumia na kujiajiri, lakini wengi hutegemea bado kuajiriwa, na wakikosa ajira ndipo huanza kulalamika maisha magumu.

### KUWA WABUNIFU

"Dira ya maisha yenu vijana mnayo wenyewe na mkitaka utajiri msitegemee kuajiriwa, matajiri katika nchi hii na duniani kote ni wafanyabiashara, wabunifu na wajasiriamali. Waliojiriwa wanapata fedha ya kujikimu tu kimaisha, hivyo nawasihi nyie wasichana msibweteke fursa zipo zitafuteni," anasema Mwangulumbi.

Anaongeza: "Mkitaka kupata fedha za mikopo za halmashauri, bunini biashara itawakwamua kiuchumi njooni na mawazo ya kufungua viwanda vidogo siyo kulima nyanya ama kuuza mchicha na dagaa sitatoa fedha."




Ofisa Vijana Halmashauri ya Shinyanga, Charles Luchagula, anasema manispaa hiyo imetoa fedha nyingi kwa vikundi vya ujasiriamali na kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2015 hadi 2020) zimetolewa takribani Shilingi bilioni moja ili kuwainua kiuchumi.

Aidha, anasema serikali imekuwa ikiendelea kutoa elimu kwa vijana, wanawake, na watu wenye ulemavu kujiunga kwenye vikundi vya ujasiriamali, lakini mwitikio wa vijana sio mkubwa kutokana na kujenga dhana ya kutegemea kuajiriwa na kuendelea kuranda randa mitaani na wasichana kujiingiza kwenye biashara ya ngono na kuwataka kuwa wabunifu na kuachana na mazoea.

### VIJANA KUJITAMBUA

Mjumbe wa Baraza la Mashekhe Mkoa wa Shinyanga, Majaliwa Masoud, anawasihi vijana hasa wasichana ambao hawana kazi, wachangamkie fursa za mikopo ya halmashauri kwa kunzisha mawazo ya kibiashara yanayovutia ikiwamo kufungua viwanda vidogo, ili wapate fedha na kuendeleza maisha yao.

Anasema ni wakati wa vijana kujitambua na kuacha kujidharau kuwa hawawezi, ikiwa serikali imeshawawekea mazingira wezeshi ya kufanya biashara mbalimbali na kujikwamua kiuchumi na kuwataka kuchana na tabia ya kuranda randa mitaani wakati kuna fursa nyingi za kuwaingizia kipato.

ELIMU
**NA GAUDENSIA MNGUMI**

# TAS inavyopambana na saratani ya ngozi, yasambaza mashine kutoa tiba

HALI ya ualbino inasababishwa na kukosa au kuwa na upungufu wa rangi ya asili kwenye macho, nywele na ngozi, hivyo wanaoishi na ualbino (PWA) ngozi yao kuumizwa kiurahisi na mionzi hatarishi ya jua na kusababisha saratani ya ngozi.

Seif Kondo, Ofisa Ugharibishi wa Taasisi ya Under The Same Sun (UTSS), inayohusika na ustawi wa PWA, akizungumzia suala hilo, anasema mionzi ya jua kali inasababisha wenye ualbino wengi hasa vijana wenye umri wa chini ya miaka 40 kupoteza maisha kutokana na saratani hiyo.

Anasema inasikitisha kupoteza maisha katika umri huo na kukumbusha kuwa mionzi inayoumiza ngozi kitaalamu huitwa UVA na VUB na UVC ambayo inaweza kuzuiliwa isiumize wenye ualbino kwa kuzingatia haya.

"Inapowezekana PWA wasifanyekazi kwenye mazingira wala kutembea kwenye jua kali, kama si lazima waepuka. Tunashauri kutumia mavazi yanayofunika mwili mzima. Funika mikono, vaa suruali funika miguu, pia vaa mavazi yanayofunika shingo na pia kofia pana kufunika kichwa uso na macho na kikubwa ni kupunguza kukaa, kutembea na kufanyakazi juani kama siyo lazima," anasema Kondo.

**MAFUTA MAALUMU**

Kondo anawashauri wenye ualbino kutumia mafuta kinga yanayozuia mionzi hatarishi yaitwayo 'sun screen' ili kuizuia isipenye mwilini.


Anawaelekeza kuyapaka mikononi, usoni, miguuni na sehemu zinazoweza kufikiwa na jua na kufanya hivyo mara mbili kwa siku, kupaka dakika 10 kabla ya kuondoka nyumbani na baadaye kutegemeana na hali ya jua wakati wa kurudi.

**ANGALIZO**

Ofisa Uraghibishi anawashauri wanaoishi na ualbino kununua mafuta kinga yenye kiwango cha kuzuia mionzi hatari 'SPF' kikubwa kiwe kati ya 30 hadi 100.

Anakumbusha kuwa SPF ni 'sun prevention factor' umahiri wa kuzuia jua na kama ilivyo kwa vitakasa mikono kuzuia corona, ni lazima 'sanitaiza' iwe na zaidi ya pombe (alcohol) asilimia zaidi ya 50, vivyo hivyo kwa mafuta kinga, SPF iwe zaidi ya asilimia 30.

Anasema mafuta hayo ni ghali, lakini jitihada zinafanywa na hata UTSS inayatoa kuwasaidia wanaoyahitaji ili kunusuru maisha kwa kuwa hiyo ni dawa ili kulinda maisha.



Abdallah Badilia, akiwa kwenye moja ya mikutano ya asasi za kiraia kuzungumzia masuala ya ustawi wa jamii. **PICHA: MWANDISHI WETU**

**TASS INASAMBAZA TIBA**

Katika jitihada za kukabiliana na saratani ya ngozi, Chama cha Wenye Ualbino Tanzania (TAS) kimesambaza mashine za kutoa mionzi kwenye hospitali nyingi za serikali.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa TAS Godson Mollel, mashine zimefungwa hospitali za rufani za mikoa ya Singida kuhudumia wanachama na wagonjwa wengine wa mkoa wa Dodoma, Singida, Tabora.

Aidha, zimefungwa katika Hospitali ya Mkoa wa Lindi kuwafikishia huduma kwa PWA walioko Mtwara wakati nyingine imefungwa Tanga, nyingine iko Iringa, Morogoro na wanaoishi Pemba na Zanzibar wamefikishiwa huduma ya mashine ya kutoa mionzi.

Anasema kusogeza huduma hizo karibu na wananchi ni zoezi endelevu mashine zitaendelea kupelekwa kila zinapopatikana kwenye hospitali za serikali na kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, ili kuwasaidia PWA na jamii ikiwamo kinamama wenye saratani ya shingo ya kizazi.

"Tunatoa huduma hii ya 'cryogenic equipment' ni mashine za kutoa mionzi. Tunazipata kutoka Afrika Kusini. Gharama zake ni takribani Shilingi milioni 10. Tunasogeza huduma karibu ili PWA wanaoathirika na saratani ya ngozi wapate huduma karibu kwani wapo wanaoshindwa kusafiri kutoka mikoani hadi Taasisi ya Tiba ya Saratani Ocean Road."

Anapoulizwa kuhusu wataalamu anasema wapo na wamepata mafunzo ya kutoa huduma hiyo ya tiba ya mionzi.

**MAFANIKIO**

Mollel anasema yapo na wanachama wamefahamu wanachunguzwa na wengi wanaendelea kutumia huduma hiyo, japo haikuwa rahisi kupata takwimu za moja kwa moja.

**CHANGAMOTO**

Anasema PWA hawakai sehemu moja wametawanyika, wengine wanaishi mbali mno na miji wanaweza kuwa na maradhi lakini wakakosa nauli ya kufika hospitalini na kuoimba serikali isaidie kwa kutenga bajeti ya kuwasaidia wahitaji hasa kutoka familia maskini.

Anaomba Idara za Ustawi wa Jamii zilizoko kila kata ziwafikie na kuwatambua, ili serikali isaidie kuwapatia usafiri wafike hospitalini hasa siku za kliniki kuchunguzwa na kutibiwa.

"Siyo serikali pekee tunaomba wadau wote asasi za kiraia, taasisi za kidini, shule za umma na binafsi kuunga mkono kuwafikia wanaoishi na ulbino hasa wa familia maskini ili wapate tiba ambayo hutolewa bure, " anasema Mollel.

Anaamini serikali inaweza kuwasaidia wenye ualbino kwa sababu kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya 2012, idadi ya PWA nchini ni takribani 18,000 idadi ambayo inaweza kuigharamia.

**USHAURI KWA TAS**

Abdallah Badilia ni mwanafunzi wa shahada ya kwanza akisoma Chuo Kikuu cha Diplomasia Dar es Salaam, anayezungumzia jitihada hizo na kushauri mambo kadhaa.

Anapongeza juhudi za TAS na UTSS na kuhimiza kuwahamasisha watu ili wafahamu, kuwapo kwa tiba ili wawahi hospitalini, wachunguzwe na kutibiwa mapema.

Ana wasiwasi kuwa PWA wengi hawafahamu, akijitolewa mfano kuwa wakati anaishi Dar es Salaam, hafahamu kuhusu kusambazwa mashine za kutoa mionzi mikoani.

Badilia ana wasiwasi kuwa watu wengine wanaoishi mbali zaidi wanaweza wasifahamu hivyo wasinufaike. Badilia anayeishi na ualbino anashauri kutangaza zaidi uwepo wa huduma hizo hasa vijijni kwa kutumia mawasiliano kwenye kliniki za wajawazito, hospitalini, kuweka mabango ofisi za vijiji, shuleni na pia vyombo vya habari hasa redio za kijamii ambazo anaamini zinawafikia watu wengi.

Akijibu hofu hiyo, Mwenyekiti wa TAS Mollel alisema chama kina viongozi kila mkoa na wilaya na wanafanya jitihada kuwafikia na kuwafahamika wanachama wao.

# TEHAMA MAHAKAMANI

**INATOKA UK.11**

Aidha, anasema, hatua hiyo inachangia kulinda usalama wa shahidi asiwe mwoga pale anapokutana na mhalifu wake na pia huondoa mianya ya rushwa na visingizio visivyo na msingi.

Anataja visingizo hivyo kuwa ni jalada kutoonekana, kupotea, kucheleweshwa au kuzungushwa, katika upatikanaji wa nakala ya hukumu na pia TEHAMA inarahisisha usikilizwaji wa kesi kwa haraka, na hakimu anaweza kusikiliza kesi nyingi zilizo katika mahakama tofauti bila yeye kwenda katika maeneo husika.

"Mahakama ina mifumo mbalimbali inayorahisisha upatikanaji wa haki, na baadhi yake ni kusikiliza mashauri kwa njia ya video (Video Conferencing), mfumo wa kuwatambua mawakili (TAMS-Tanzania Advocates Management System), na ule wa kusajili mashauri (JSDS ll (Judicial Statistics Dashboard System)," anasema.

Jaji Kiongozi huyo, anawataka watumishi wa mahakama kuwa wepesi katika kujifunza mifumo ya mahakama na pia kuhakikisha wanapata taarifa mbalimbali za shughuli za mahakama kupitia mifumo mingine ikiwamo tovuti, blog, twitter na facebook.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU, ARUSHA

## UTUMISHI HLRC MIAKA 22

# Dk. Hellen Kijo - Bisimba atoa ushuhuda unaochoma, kuonya na kutaka kazi zaidi

"KATIKA maisha yangu sehemu ya utetezi wa haki za binadamu, kusimamia, kuheshimiwa na kuthamini utu wa mtu limekuwa jukumu kubwa. Kama si kuumwa na kustaafu huenda pengine ningekuwa bado kazini."

Ni Dk. Helen Kijo-Bisimba, mwanzilishi wa asasi za kiraia zinazotetea haki za binadamu ambaye kitaaluma ni mwalimu. Hata hivyo, baada ya kusoma sheria anaangukia upande mwingine. Ni gwiji la kutetea haki za binadamu na mhamasishaji, 'lobist' wa mabadiliko ndani ya jamii.

Anasema hayo akizungumza na kusanyiko la asasi za kiraia za Afrika Mashariki zinazojumuisha karibu sekta zote pamoja na wanahabari, lililokutana jijini Arusha.

Anatoa uzoefu kwenye mjadala wa kurithishana kutoka kizazi kimoja kwenda kingine, kwenye mkutano uliondaliwa na Action Aid Tanzania na wadau wake.

Anasema alipomaliza masomo ya sheria chuo kikuu, miaka ya 1990 anashiriki kuanzisha Shirika la Wanawake Wanasheria (WILAC) lakini haishii hapo anasonga mbele kuanzisha Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC).

"Kinaposimama ninakuwa mkurugenzi wa kwanza nikafanyakazi kwa miaka 22. Wakati huo sikujua kuwa kuna likizo au kupumzika. Muda wote ulikuwa kuwahudumia wananchi. Sikuvutiwa na kingine zaidi ya kujitolea na kusaidia wenye matatizo hasa kukosa haki za msingi, kuumizwa, kukosa utetezi." Anasema, mwanasheria huyo ambaye sasa amestaafu.



Dk. Hellen Kijo-Bisimba, akizungumza na wadau wa asasi za kiraia (hawako pichani), mjini Arusha hivi karibuni. **PICHA: MWANDISHI WETU**

### YALIYOMUUZA ZAIDI

Anasema: "Nimetembea karibu Tanzania nzima. Nimesikia na kufahamu mengi yaliyonistua na kuniduwaza na kujiuliza hivi hapa ni Tanzania au ni dunia gani? Ni pale nilipofika Ukerewe nikaambiwa kuna mila ya kutakasa wajane mwaka 2003. Nami ni mjane ikabidi nifuatilie zaidi. Niliumia niliyoyasikia," anasema Dk. Kijo-Bisimba.

Anaeleza kuwa kutakasa wajane ni utaratibu wa kutafuta mwanaume anayeitwa 'mwesha au mtakasaji' baada ya mjane huyo kufiwa. Anamwingilia kwa nguvu ili kumwondolea mikosi.

Anasema jambo hilo liliwadhalilisha wanawake kwa vile kwa yeyote aliyefiwa baada ya mazishi jamaa zake walimtafutia 'mwesha' na kwamba kwa baadhi ya maeneo walikuwapo watu maalumu kufanya jukumu hilo.

"Ni watu waliokuwa wamechanganyikiwa ni kama akili zao haziko sawa. Walikuwa wakitafutwa kuwaingilia wajane kwa nguvu licha ya kuwapo maradhi hasa UKIMWI."

Anasema kama mjane aliumizwa na matendo hayo kwani kufiwa ni uchungu mkubwa, kuachiwa familia pengine bila kujua cha kufanya kunaongeza maumivu zaidi. Lakini aliguswa na ukatili huo ambao kwa wengine walijipatia mapato kwani mwesha alikuwa analipwa.

"Wapo wanaodai pesa nyingi kisa wanawatakasa wajane," anasema Dk. Hellen.

### UDHALILISHAJI MKUBWA

Pamoja na kufiwa ukikataa unatengwa na jamii. Huwezi kwenda kusaga mahindi, kisimani kuchota maji na shughuli nyingine za kijamii kama sherehe, misiba na ibada.

### UFUMBUZI ALIOUFIKIRIA

Dokta Bisimba anasema ni pamoja na kuwapo sheria kali za kuwalinda wajane na kupiga marufuku ubakaji wa wanawake wanyonge kama wafiwa hao kwa kisingizio cha mila na desturi.

"Inawezekana kwa kuboresha sheria ya makosa ya kujamiiana (SOSPA) na kuingiza vipengele vipya, ili kupinga mila hizo kisheria ambazo nilisikia zinafanywa mikoa ya Mara na Tanga kwa siri."

### KUSHTAKI VIONGOZI WAKUU

Anazungumzia LHRC kuwachukulia hatua ili kuwakumbusha viongozi wakuu wa serikali kuwa wanatakiwa kuheshimu sheria, katiba na taratibu za za nchi, akitoa mfano kuwa LHRC na wadau walimshtaki Waziri Mkuu Mizengo Pinda kwa maneno yaliyokiuka haki za binadamu na katiba.

Akiwa bungeni Pinda, aliwaagiza polisi kuwapiga wote wanaokiuka amri za serikali akisema 'wapigwe tu, watapigwa tu'. Kituo hicho kilihoji iwapo maelekezo hayo yanalindwa na kinga iliyoko kikatiba.

Kesi hiyo ilitupiliwa mbali na Mahakama Kuu kwa maelezo kuwa washtaki hao walitakiwa kuonyesha jinsi wao binafsi walivyoathiriwa na maelekezo hayo.

### UKEKETAJI MOROGORO

Dk. Kijo-Bisimba, anazungumzia moja ya mafanikio yaliyofanikisha ni kubadili jamii, akitaja tukio ambalo HLRC ilihusika kuwashtaki wazazi waliokeketa mabinti na kuleta mabadiliko kifamilia.

Anasema ni mkasa uliotokea Morogoro, kulikuwa na mabinti waliokimbia kuketwa na kuozwa. Wakambilia kanisani kwa mchungaji aliyekuwa jamii ya Wamasai. Akawapeleka polisi na viongozi wengine wa serikali waliowarudisha kwa familia zao kwa maelezo kuwa waacheni watu waendelee na mila zao.

"Viongozi wa mkoa na wilaya na polisi waliwarejesha kwa familia zao na wakakeketwa kwa maelezo kuwa waacheni watu na mila zao. Ni jambo la kushangaza wakati kulikuwa na sheria ya makosa ya kujamiiana SOSPA iliyokuwa inakataza ukeketaji na ubakaji. Tuliipata tuliomba kufanya upelelezi binafsi na kufungua mashtaka. Tuliruhusiwa na kuwafikisha mahakamani washtakiwa. Japo kesi iliishia njiani kutokana na kukosa ushahidi. Baba wa mabinti waliokeketwa alijua sheria, ubaya wa ukeketaji na kulifahamu kosa lake na kujiunga na wanaharakati wa kupinga ukeketaji akihamasisha mabadiliko baada ya kujua kuwa ni jinai."

### KUTETEA WAFANYAKAZI

Wakati huo uwekezaji ukipamba moto, Dk. Bisimba anasema walikuwapo wawezekezaji ambao waliwapa wafanyakazi mikataba ya 'ajabu'.

Ilikuwa imeandikwa kwa lugha ambayo si Kiswahili wala Kiingereza. Ilibidi kuutafsiri kwa wakalimani na kujua maana yake na kuwasaidia wafanyakazi kudai haki zao.

Anasema hatua hiyo ilibadilisha mienendo ya ajira na kuheshimu haki za wafanyakazi ambao wengi walihamasishwa na kuanza kudai haki zao kisheria wakisaidiawa na HLRC.

### LHRC KUWAFIKIA POLISI

Dk. Bisimba anaeleza kuwa katika jitihada za kuishirikisha polisi kutetea haki za binadamu, alihusika kuwapa mafunzo ya haki za binadamu makamanda wa polisi (OCD) karibu mikoa yote.

Uhamasishaji huo uliongeza kasi ya kutetea na kulinda haki za watoto, wanawake na wengine kupitia uanzishwaji wa madawati ya jinsia kwenye vituo vya polisi hapa nchini.

Anasema LHRC imeanzisha klabu za kutetea haki za binadamu kwa kushirikiana na vijana, lakini kusambaza wasaidizi wa kisheria (para legals) na wafuatiliaji wa haki za binadamu katika msingi ya Tanzania.

### MSAMIATI HAKI

Dk. Bisimba anasema kutamka neno 'haki' zamani hizo ilikuwa kama 'uhaini,' lakini leo haki ni kama 'housestyle (msamiati wa kila mmoja,' kila mtu anazungumzia haki.

Anasema alifanikiwa kwenye kazi kwa kuwa kila kitu alilichokifanya kilipata nguvu ya wananachi ambao walimtetea na kila alichokifanya na kusimamia alihakikisha kinakuwa cha kweli baada ya kufanya utafiti pamoja na kupata ushahidi wa kutosha.

"Sina cha kuogopa japo nilikuwa nafuatiliwa na kutishwa kwa sababu tulifuata sheria na kusimamia ukweli. Hata wakati wa mgomo wa madaktari Hospitali ya Muhimbili niliona magari yanatufuata hadi nyumbani Kurasini. Sikutishika na vitisho na katika suala hilo la Muhimbili niliongea kwa ukali sana."

Anasema walitembelea hospitali na tukakuta miili haijaondolewa wodini kwa sababu hakuna daktari. Watu walikufa na serikali ilishindwa kutimiza wajibu wake.

Anakumbusha kuwa kitendo cha wanaharakati kulala barabarani Sarenda jijini Dar es Salaam na kuzuia magari kililazimisha serikali kuwasikiliza madaktari na ufumbuzi kupatikana. "Woga hausaidii." Anakumbusha.



## Aweso aagiza kuchimbwa visima vikubwa 2

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Juma Aweso, amemwagiza Katibu wa wizara hiyo, Antony Sanga, kuhakikisha Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA), inachimba visima viwili vya maji vyenye uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 400 kila kimoja, ili kukidhi ongezeko la mahitaji ya maji kwa wakazi wa Jiji la Dodoma.

Idadi hiyo itafanya Dodoma iwe na visima vitatu vikubwa vyenye uwezo wa kuzalisha mita za uzajo 1,200 sawa na lita milioni 1.2 kwa saa maji ambayo yatakidhi mahitaji ya wananchi wa jiji hilo.

Akizungumza katika ziara ya kushtukiza ya ujenzi wa kisima cha maji unaoendelea katika eneo la Mzakwe, Aweso alisema hivi sasa Dodoma kuna upungufu wa maji mita za ujazo 21,000. Alisema kutokana na uwezo wa Dodoma hivi sasa kuzalisha mita za ujazo 66,000 wakati uhitaji uliopo ni mita za ujazo 103,000, visima hivyo vikiongezwa vitasaidia kuziba pengo hilo linalosababisha maeneo mengine kukosa maji.

"Hivi sasa Dodoma tunauwezo wa kuzalisha mita za ujazo za maji 66,000 wakati hitaji la maji ni mita za ujazo 103,000, hivyo tunahitaji kuziba pengo hilo, ndiyo maana naagiza visima hivyo vichimbwe," alisema Aweso.

Hata hivyo, alisema imefika wakati sasa ujanja ujanja uliokuwa ukifanyika kwa wataalamu wa maji katika halmashauri na sehemu nyingi kufikia mwisho na kila mmoja anapaswa kufanya kazi kwa bidii ili kila eneo wapate maji.

Alisema visima hivyo vyote vikikamilika, kutakuwa na uwepo wa maji lita milioni 28 kwa saa na kuongeza kuwa ili kuhakikisha wanamaliza tatizo la maji, DDCA inatekeleza uchimbaji wa visima 10 eneo la Zuzu na Chamwino.

"Naagiza wakazi wote wapate maji sawa na kwa wakati siyo eneo lingine unakuta watu wanapata maji wengine wanakosa, maji ni muhimu mtu akikosa inaweza sababisha kupata maradhi," alisema Aweso.

Katibu wa Wizara ya Maji, Sanga, alisema lengo la ziara hiyo ni kujiridhisha ahadi iliotolewa na DUWASA ya kufanya kazi usiku na mchana ili kukamilisha ujenzi wa kisima hicho ndani ya siku 60.

# Mwambe ataka mageuzi kuibua wawekezaji wapya

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Geoffrey Mwambe, amewataka watendaji katika wizara hiyo kufanya kazi kwa weledi na ubunifu mkubwa, ili kuleta mageuzi katika wizara na kuongeza uwezo wa kuibua wawekezaji wapya wazawa nchini.

Waziri Mwambe, alitoa wito huo jijini hapa wakati akifungua mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa wizara hiyo.

Alisema kila mtendaji na wakuu wa idara katika wizara wanatakiwa kuhakikisha wanafanyakazi kwa bidii na kuibua wawekezaji wapya.

"Kila mtumishi katika kitengo chake au idara afanyekazi kwa weledi mkubwa natamani mabadiliko makubwa na kwa muda mfupi kila mtendaji ujitambue na ujitafakari utalifanyia nini taifa lako," alisema.

**Kila mtumishi katika kitengo chake au idara afanyekazi kwa weledi mkubwa natamani mabadiliko makubwa na kwa muda mfupi kila mtendaji ujitambue na ujitafakari utalifanyia nini taifa lako.**

Alisema nchi ina fursa nyingi ambazo zingewanufaisha Watanzania, lakini walioaminiwa kusimamia vitengo hivyo bado hawajafanya kitu cha ajabu ambacho kitawanufaisha katika sekta hiyo.

Waziri Mwambe, alisema wizara ndiyo wahamasishaji na wawezeshaji wa shughuli za viwanda nchini, wanatakiwa kujitoa kwa nguvu zao zote na akili kuhakikisha sekta hiyo inakua na kuwanufaisha Watanzania.

Alitaka kuboreshwa kwa kitengo cha huduma kwa wateja katika wizara, ili kuwakaribisha wawekezaji na siyo kutoa kauli mbaya kwa wateja wanaohitaji huduma.

Aliwataka watendaji na wasimamizi katika wizara kujenga utaratibu wa kuwapa motisha wafanyakazi wanaofanyakazi kwa uaminifu ili kuwaongezea motisha kwa kuwa jitihada hizo zitahamasisha utendaji kazi katika wizara na kusimamia ushirikishwaji kwa watumishi wote katika majukumu.

"Katika hili hakikisheni ushirikishwaji kwa watumishi na kugawa majukumu sawa kwa watumishi wote na kutowabagua kitendo cha kuwabagua au kutoa majukumu kwa upendeleo itashusha morali kwa watumishi," alisema.

Pia, alihamasisha wakuu wa idara kutoa nafasi kwa watumishi wao kujiendeleza kimasomo kusaidia kuimarisha watumishi kuwapanua kimawazo na kuwapandisha katika nafasi zao.

"Nina ushahidi wapo walioanza kazi kama masekretari katika ofisi, lakini wakajiendeleza na hatimaye wakaja wakawa wakuu wa idara, kwa hiyo unaweza ukaanza kama dereva, lakini ukamaliza kama katibu mkuu hiyo ni heshima kubwa sana," alisema.

Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Profesa Rikizi Shemdoe, alisema mkutano huo ni wa pili tangu kuzinduliwa kwa baraza hilo na utatumika kutathmini waliyokubaliana katika mkutano wa kwanza na kuweka mikakati mipya ya kutekeleza kwa mwaka huu.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi ya Umma, Deogratius Ndejembi (kulia), akiangalia gari ambalo haikujulikana ni aina gani kama alivyoikuta katika kijiji cha Membe, Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma, mwisho wa wiki kwenye ziara yake, magari hayo yanatengenezwa kijijini hapo kwa ajili ya kusafirisha mazao kutoka mashambani kupeleka kijijini hapo na vijiji vya jirani. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Jafo asisitiza ubunifu wahitimu Chuo cha Mipango

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, amewataka wahitimu wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini (IRDP), kuwa wabunifu katika mipango ya maendeleo kwa kutumia elimu waliyoipata.

Alitoa rai hiyo alipokuwa akizungumza na wahitimu wa chuo hicho baada ya kutunukiwa vyeti kwenye mahafali ya 34, yaliyofanyika jijini hapa.

Alisema, badala ya kusubiri kuajiriwa watumie elimu waliyoipata kuwa wabunifu katika mipango ya maendeleo, ili kujiletea maendeleo yao binafsi na jamii inayowazunguka.

Aliwataka wahitimu hao kuhakikisha wanakuwa vielelezo vya kutunza na kuenzi amani ya taifa.

Mkuu wa chuo hicho, Prof. Hozen Mayaya, alisema kwa mwaka wa masomo 2018/2019, kampasi kuu imekuwa na ongezeko kubwa la udahili wa wanafunzi wapya kutoka wanafunzi 4,317 mwaka 2019/2020 hadi 5,856 ikiwa ni ongezeko asilimia 26.

Prof. Mayaya alisema kuwa idadi ya wahitimu imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka na kwa mwaka 2020 jumla ya wahitimu 4,072 wamehitimu kwa fani mbalimbali ikiwa ni ongezeko la asilimia 27.

Prof. huyo alitaja miradi mingine ni pamoja na kuwajengea uwezo watumishi wake wa mamlaka za serikali za mitaa za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar uliofanyika mwaka 2018, Agosti hadi Julai 2021.

Alisema, mradi huo pia wa kuwajengea uwezo watumishi wa mamlaka za serikali za mitaa, katika uandaaji wa mipango na bajeti imefanyika ambao unaozingatia mahitaji ya watoto uliofanyika Agosti 2018-Julai 2021.

Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa Chuo hicho, Prof. Martha Qorro, alisema chuo kinakabiliwa na upungufu wa watumishi kada ya wahadhiri kila mwaka kutokana na kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaojiunga.

Alisema hadi kufikia Novemba 2020, chuo kilikuwa na upungufu wa wahadhiri 81 na kwa sasa kuna wahadhiri 132, idadi ambayo haitoshelezi kulingana na wanafunzi waliopo zaidi ya 10,000.



# Wakulima kunufaika maonyesho kilimo biashara

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKULIMA zaidi ya 4,000 wanatarajia kunufaika na maonyesho ya kilimo biashara ambayo yatahusisha mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, lengo kuu likiwa ni kuwasaidia wakulima kujikwamua kiuchumi.

Maonyesho hayo yatafanyika mkoani hapa kwenye mashamba ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kituo cha Uyole Mei, 2021.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maonyesho hayo, mtafiti wa mazao ya mahindi, maharagwe na soya ambaye ni mratibu wa maonyesho hayo, Leonard Sabula, alisema wakulima wapatao 4,000 watashiriki.

"Maonyesho ya awamu hii yatakuwa ya aina yake maana tumefanya maboresho makubwa na kuwahusisha wadau wengi, hadi sasa kampuni zaidi ya 20 zikiwamo za pembejeo za kilimo na biashara zimethibitisha kushiriki, nina imani wakulima watajifunza masuala mbalimbali ya kuongeza thamani katika mazao yao pia kupata masoko ya uhakika," alisema Sabula.

**Maonyesho ya mwaka jana wadau 698 walishiriki wakiwamo wanaume 371 na wanawake 327, ambao walijifunza mbinu mbalimbali za kilimo bora.**

Aliongeza kuwa kwa mwaka huu walishindwa kufanya maonyesho hayo kutokana na uwapo wa mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona, ambao ulisababisha maandalizi kukwama kutokana na wadau kulalamikia ukata wa fedha.

Sabula alibainisha kuwa maonyesho ya mwaka jana wadau 698 walishiriki wakiwamo wanaume 371 na wanawake 327, ambao walijifunza mbinu mbalimbali za kilimo bora.

Mkurugenzi wa TARI Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema maonyesho ya kilimo biashara yanalengo la kuongeza mnyororo wa thamani kwenye mazao.

Alisema kupitia maonyesho hayo wadau wanapata fursa ya kuonyesha teknolojia zao kupitia mashamba darasa au vipando vya aina mbalimbali za mazao waliyoyapanda, ambayo wanatumia kuwafundisha wakulima wanaotembelea.

Aliwahamasisha wakulima kutoka maeneo mbalimbali kutembelea maonyesho hayo ambayo yatakuwa na tija kwao, kwa kuwa watajifunza mbinu za utayarishaji wa mashamba, upandaji mazao, kuvuna kwa njia za kisasa.

Wadau wa kilimo ambao ni washirika wa maonyesho hayo, akiwamo Prudence Gerald, Ofisa Programu kutoka Baraza la Nafaka Ukanda wa Afrika Mashariki, alisema ni msimu wa pili tangu kuanzishwa kwa maonyesho hayo na yamebadilisha mtazamo wa wakulima wengi kutoka kulima kilimo cha mazoea hadi uzalishaji wa teknolojia.

Alisema baraza hilo limekuwa likiwaunganisha wakulima na masoko mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi pamoja na kuwashauri ni aina gani ya mazao ambayo yanafaida.

## Mafuta ya kula yaadimika madukani

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

LICHA ya serikali kutoa maelekezo kuhusu bei elekezi ya mafuta ya kula na kuwahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao ya alizeti na ufuta, bado kuna uhaba wa malighafi hiyo mitaani.

Utafiti uliofanywa na Nipashe katika baadhi ya maduka umebaini kati ya maduka 10 ya kuuza mafuta ni mawili pekee ambayo yana malighali hiyo kwa kipimo cha kuanzia lita tatu hadi 10.

Pia, katika maeneo mengine malighafi hiyo inapatikana kuanzia lita 10 jambo ambalo linawaumiza wananchi wenye kipato cha chini ambao uwezo wao ni kumudu mafuta ya kuanzia lita tatu au moja.

Katika Soko la Sido ambalo lina mashine nyingi za kukamua mafuta ya alizeti, Nipashe ilishuhudia idadi ndogo ya malighafi hiyo, kinyume na ilivyozoeleka.

Akizungumza na Nipashe, Severine Mwakyusa mkazi wa Isanga alisema alizoea kununua mafuta ya kula lita tatu, lakini kwa sasa kiasi hicho madukani kimeadimika na analazimika kununua kuanzia lita tano ambayo kwa sasa huuzwa Sh. 24,000 huku lita 10 ikiuzwa Sh. 35,000.

Mwakyusa alisema alizoea lita tatu kununua kwa Sh. 12,000 ambayo kwa sasa inauzwa kwa Sh. 13,500 na kupatikana ni tatizo.

Kutokana na hali hiyo, Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania TARI, Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema tayari wamezalisha miche ya alizeti, soya, na michikichi na kuwataka wakulima wafike kituoni hapo ili kuichukua.



Mwangalizi wa Makanisa ya Pentecostal Holiness Association Mission (PHAMT), Mchungaji Dk. Benjamin Kiwovere (kulia), akimkabidhi katiba ya kanisa hilo, Mchungaji Justine Mdede ambaye alisimikwa juzi, Uyole Njia Panda. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Askofu ashauri waumini kujiepusha siasa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ASKOFU wa Kanisa la Pentecostal Holiness Association Mission Tanzania (PHAMT), Nkumbu Mwalyego, amewashauri waumini wa kanisa hilo kuachana na masuala ya siasa kwa madai kuwa yanasababisha makundi na mipasuko ndani ya kanisa.

Alitoa rai hiyo wakati wa ibada ya kumsimika Mchungaji wa Kanisa hilo, Justine Mdede, kuwa kuna baadhi ya waumini wanajihusisha na masuala ya siasa na kutumia nguvu kuwavuruga waumini wengine na kusababisha kumkosea Mungu.

Alisema waumini wanapaswa kuwa na misimamo katika kumtumikia Mungu kwa kutokubali kuyumbishwa na baadhi ya watu wasiolitakia mema kanisa hilo na kuwa wajasiri kupinga viashiria vyovyote vya kuwagawa.

"Utumishi wa Mungu unahusu masuala ya rohoni sio kisiasa, ukiamua kumtumikia lazima ujikane na mambo yote ambayo yatachangia kumkosea ikiwamo siasa, kuweni majasiri, mkemee na mwonyeshe msimamo kwa wale wote watakaojaribu kuwagawa, zaidi mpatieni ushirikiano wa kutosha mchungaji huyu ambaye leo amesimikwa kwa ajili ya kazi ya bwana," alisema Askofu Mwakyego.

Alimshauri Mchungaji Justine Mdede ambaye alisimikwa tayari kwa ajili ya kazi ya uchungaji kuhakikisha anasimama katika misingi ya kanisa na kutokuwa sehemu ya migogoro.

Pia, alimshauri kuvumilia, kukemea na kuonywa kwa upendo dhidi ya muumini yeyote atayekwenda kinyume na maadili ya kanisa na kwamba asiogope lawama wala cheo cha mtu.

Mwangalizi wa Makanisa ya PHAMT, Jimbo la Mbeya, Mchungaji Dk. Benjamin Kiwovere, alisema kiongozi yeyote akikubali wito wa kuwa mchungaji hapaswi kutanguliza fedha mbele kuliko kazi ya Mungu.

Alisema mchungaji anapaswa kujitolea na kuwa na upendo kwa kazi yake ili kujiepusha na tamaa pamoja na mitego itakayomwingiza kwenye dhambi.

Baadhi ya waumini wa kanisa hilo, akiwamo Grace Shaula, waliahidi kumpa ushirikiano mchungaji aliyesimikwa kwa kutokubali kuona mtu anawashawishi kuleta chuki na mpasuko.

Alisema wako kwa ajili ya kumtumikia Mungu na wana imani kubwa kwa Mchungaji Mdede kuwaongoza kwenye njia ya kumpendeza Mungu.



# UVCCM yatakiwa kuibua miradi ya kimaendeleo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BARAZA Kuu la Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) Mkoa wa Kusini Unguja, limetakiwa kuibua miradi ya kimaendeleo itakayowanufaisha vijana katika harakati zao za kujiimarisha kiuchumi.

Hayo yalielezwa jana na Naibu Katibu Mkuu UVCCM Zanzibar, Mussa Haji Mussa, alipokuwa akizungumza na wajumbe wa baraza hilo Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema endapo miradi ya kimaendeleo itaanzishwa na kuwafikia vijana itakuwa rahisi kupunguza kundi kubwa la vijana wanaosubiri ajira kutoka serikalini.

**Endapo miradi ya kimaendeleo itaanzishwa na kuwafikia vijana itakuwa rahisi kupunguza kundi kubwa la vijana wanaosubiri ajira kutoka serikalini.**

Aliwataka viongozi wa Mkoa wa Kusini kuwa mstari wa mbele kutoa kipaumbele fursa za kuwawezesha vijana kujiajiri kwa kuwa serikali haina nafasi za ajira kwa vijana wote.

Pia, alisema Mkoa wa Kusini unaongoza kuwa na viongozi wengi waliotoka UVCCM na kupata fursa katika vyombo vya uamuzi ikiwa ni pamoja na ubunge, uwakilishi na udiwani na kuwataka viongozi hao kusema tatizo linalowakabili vijana ili wapatiwe ufumbuzi wa haraka.

Aliwataka vijana wa UVCCM mkoani humo kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ziwe za chama au serikali ili kupeleka mbele harakati za kuwapigania vijana wenzao.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa wa Kusini Unguja, Latifa Khamis Juakali, alisema baraza litahakikisha linaanzisha miradi ili vijana wanufaike na miradi hiyo huku akiwapongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar kwa kuwaamini vijana katika serikali.

Akitoa taarifa ya UVCCM Mkoa wa Kusini Unguja, Katibu wa UVCCM wa mkoa huo, Aboud Said Mpate, alisema umoja wa vijana umechochea mafanikio mbalimbali ya Chama Cha Mapinduzi ikiwa ni pamoja na ushindi wa uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, kuanza kwa ujenzi wa nyumba ya mtendaji mkuu wa UVCCM Mkoa wa Kusini pamoja na kuwaunganisha vijana wa makundi mbalimbali.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman (kushoto), Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi, Idrisa Kitwana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Dk. Khalid Salum Mohamed, wakiangalia baadhi ya machapisho ya vitabu mbalimbali vilivyotungwa na waandishi mahiri wa Kiswahili. **PICHA: OMPR**

## Waziri ahimiza kumbukumbu kuenzi utamaduni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, amesema ili jamii iendelee kuenzi utamaduni wa nchi yao ipo haja ya kuwa na kumbukumbu itakayosaidia kizazi kilichopo kujua jamii yao ilikotokea, ilipo sasa na inakoelekea.

Alisema hayo juzi wakati wa tamasha la utamaduni la Mswahili huko Kiponda Mjini Unguja.

Alisema watoto kujua utamaduni wa jamii zao ni kitu kizuri ambacho kitaendelea kulinda tamaduni hasa za Afrika.

Alisema kupitia wizara yake atahakikisha anashirikiana na wasanii wa Zanzibar kukuza utamaduni wake kwa kuonyesha kazi zao.

Aliwasisitiza wasanii hao kuongeza ubunifu katika kazi kwa vile ni muhimu na kutawasaidia kuendelea kupata fursa za kushiriki maonyesho mbalimbali ambayo italikuza Taifa la Zanzibar na utamaduni wake.

Simai alisema muda umefika sasa kwa tamaduni za Zanzibar kujitangaza kupitia maeneo ya wazi kwa kuihamasisha jamii kushiriki katika matamasha ya kuonyesha utamaduni hasa wa mswahili wa Zanzibar.

Kwa upande wake Mbunge wa Jimbo la Malindi, Suleiman Omar, alisema tamasha hilo litasaidia jamii hasa wanafunzi kutambua kazi za ufundi wa vitu vya asili, wanafunzi watakapopata elimu hiyo itasaidia jamii kulinda utamaduni wao na kujiendesha kimaisha kupitia kazi za mikono.

Katika tamasha hilo vitu vyenye asili ya mswahili vilionyeshwa ikiwamo sanaa ya ufinyanzi, ushoni na uchoraji.

**Watoto kujua utamaduni wa jamii zao ni kitu kizuri ambacho kitaendelea kulinda tamaduni hasa za Afrika.**

# Mbunge awapa ushauri wajawazito kupunguza vifo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MBUNGE wa Viti Maalumu Mkoa wa Kaskazini Unguja, Sada Mansour, amewataka wajawazito kuzitumia huduma za kujifungua katika Hospitali ya Wodi ya Kivunge ambayo lengo lake ni kupunguza vifo vya watoto na kinamama.

Alisema sehemu salama ya kujifungua ni hospitali kwa sababu linapotokea tatizo ni haraka kufanyiwa kazi na wataalamu wa hospitali kuliko kujifungua kwa wakunga wa jadi.

Alitoa ushauri huo jana, wakati alipokabidhi vifaa vikiwamo vitanda kwa ajili ya wajawazito, mashuka 300 pamoja na vifaa vya tiba kwa uongozi wa Hospitali ya Kivunge vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 30.

Alisema mikakati ya Serikali ya Zanzibar ni kupunguza vifo vya kinamama na watoto na mafanikio hayo yatafikiwa iwapo watajifungua na kupata huduma katika hospitali.

Alisema amefurahishwa na mwelekeo wa hospitalini hapo ambao hivi sasa kinamama wengi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja wanajifungua katika Hospitali Kuu ya Kivunge.

"Nimefurahishwa na juhudi za kinamama sasa kupata huduma za kujifungua katika hospitali kwa sababu takwimu za miaka ya nyuma Mkoa wa Kaskazini Unguja ukiongoza kwa kinamama kujifungua majumbani," alisema.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Afya, Dk. Juma Salum Mbwana, alisema kinamama wengi wamehamasika na kuzitumia huduma za kujifungua hospitalini hapo baada ya huduma za mama na mtoto kuimarishwa.

Alisema vifaa vilivyotumiwa na mbunge wa viti maalumu vitatumika kama ilivyokusudiwa kusaidia huduma bora za kinamama wanaofika kupata matibabu.

"Tunakushukuru kwa dhati kabisa mheshimiwa mbunge kwa kuonyesha nia ya dhati ya kusaidia maendeleo ya kinamama na watoto na msaada huu tutautumia kama ilivyokusudiwa," alisema.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Jumuiya Wanawake Mkoa wa Kaskazini Unguja kupitia CCM Mariamu Shomari, alisema kilichofanywa na mbunge huyo ni kutekeleza ahadi za Ilani ya Uchaguzi ya CCM kuhakikisha serikali inapunguza vifo vya kinamama na watoto kwa kujifungua katika mazingira mazuri na salama.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:

- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:
**Dar es salaam – 0768 928 516.**
**Arusha – 0677 226 960.**

## NAFASI ZA SHULE

**Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.**

## TUNAHITAJI MAFUNDI

**TUNAHITAJI MAFUNDI WA PIKIPIKI WENYE UZOEFU, UMRI MIAKA 25-35.**
**TUMA MAOMBI KWA: linkallafrica@gmail.com**
**MWISHO WA KUTUMA MAOMBI NI: 17/12/2020.**

NIPASHE NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE NASI
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0782253676

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA KAHAMA**
**WILAYA YA KAHAMA**
**MATRIMONIAL CAUSE NO. 3 2020**

**BETINA G. LWAMUZIGU ................ PETITIONER**
**DHIDI YA**
**DANI MARTIN .................. RESPONDENT**
**KUITIWA SHAURINI**
**KWA: DANI MARTIN**
**POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake hapa mahakama ya Wilaya ya Kahama katika shauri tajwa hapo juu, ambapo ilipangwa kutajwa tarehe 21/12/2020.

Unaamriwa kuhudhuria mbele ya mahakama hii mnamo tarehe 6/1/2020, saa 2:30 asubuhi bila kukosa au kuchelewa kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutajwa shauri hilo.

Fahamu kuwa usipohudhuria siku hiyo, shauri hilo laweza kuamriwa kuendelea kusikilizwa na kutolewa hukumu upande mmoja bila wewe kuwepo.

**Imetolewa kwa AMRI yangu na CHAPA ya Mahakama hii leo 21 December, 2020.**

**C.L.Chovenye**
**Hakimu Mkazi**
**KAHAMA**

C.L.Chovenye
Hakimu Mkazi
KAHAMA
RESIDENT MAGISTRATE
KAHAMA

160494

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**KAGERA LILILOPO BUKOBA**
**MAOMBI NA:37/2020**
**CATHERINE MWAMINI JUSTUS......APPLICANT**
**DHIDI YA**
**1.JUSTUS RUTABINGWA NDIBALEMA**
**2.DEPOSIT INSURANCE BOARD.........WADAIWA**
**KWA.JUSTUS RUTABINGWA NDIBALEMA**
**(POPOTE PALE ULIPO)**

Mnaarifiwa/unaarifiwa kuwa Maombi Na 37/2020 yamepangwa kutajwa tarehe 26.01.2021 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, E.Mogasa saa 2.00 asubuhi.
Hivyo,unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/ mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.
AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MHURI wa Baraza hili leo tarehe 15.12.2020

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**BUKOBA**

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
BUKOBA

160495

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**FORM II**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA)**
**Katika Mahakama ya PONGWE**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 40/2020**
**Ombi la IDDI RASHIDI NGEREZA kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu RASHIDI MOHAMED NGEREZA**
**Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo **tarehe 31/12/2020** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo. Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 10/12/2020.**

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
PONGWE

160500

Uza,
Chenye Thamani Kubwa
Kwa
Kutangaza Nasi Kwa Bei
Poa
Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Kirusi kipya Uingereza, mkutano wa dharura waitishwa, EU yavunja safari

**London, UINGEREZA**

WAZIRI Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, jana, aliongoza mkutano wa dharura, wakati nchi kadhaa zikiendelea kuzizuia ndege zao, kwenda Uingereza.

Hatua ya nchi hizo ni kuzuia kuenea kwa aina mpya ya virusi vya corona vilivyogunduliwa nchini humo.

Johnson aliitisha mkutano wa kamati ya dharura ya mawaziri, kujadili marufuku ya safari za ndege za abiria za kimataifa.

Nchi nyingi za Ulaya, tayari zimezuia ndege na wasafiri kutoka Uingereza, huku nchi zaidi zikitarajiwa kuchukua uamuzi kama huo.

Shirika la Afya Duniani (WHO), pia limetoa wito wa hatua kali kuchukuliwa Ulaya, ambayo hadi sasa zaidi ya watu 500,000 wamekufa kutokana na ugonjwa wa COVID-19.

Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, Kansela wa Ujerumani, Angela Merkel, Mkuu wa Halmashauri ya Umoja wa Ulaya Ursula von der Leyen na Rais wa Baraza la Ulaya pamoja na Charles Michel, jana walizungumza kwa njia ya simu kuhusu suala hilo.

Nchi zaidi zinaweka vizuizi vya kusafiri kwenda na kurudi Uingereza, ikiwamo India, Hong Kong, Canada, Uswizi and Ujerumani.

Pia Ufaransa imefunga mpaka wake na Uingereza kwa saa 48, kwa malori, abiria wanaotumia Bandari ya Dover.

Nchi wanachama wa Jumuiya ya Ulaya (EU), zinakutana mjini Brussels kujadili juu ya marufuku ya safari nchini Uingereza.

Maduka makubwa ya Sainbury, nchini Uingereza, walisema kuwa vitu vinaweza kukosekana dukani mwao, kutokana na kufungwa kwa mpaka kati ya Ufaransa na Uingereza, huku wauzaji wa bidhaa za rejareja wakihofia uhaba wa chakula.

Hadi sasa duniani kote kumekuwa na kesi milioni 77 zilizothibitishwa tangu kuzuka kwa mlipuko Desemba, mwaka jana na vifo vikifikia milioni 1.7.

***DW/BBC***



Ajali iliyosababisha vifo 12 na majeruhi wanane, iliyotokea katika mji wa Joypurhat, Kaskazini mwa Bangladesh. **PICHA/TRT**

# AU yataka Kenya, Somalia kurejesha uhusiano wao

**Jibuti, DJIBOUTI**

UMOJA wa Afrika (AU), unasema hatua ya Somalia, kuvunja uhusiano wa kidiplomasia na Kenya, unahatarisha usalama na uthabiti wa eneo la Afrika Mashariki na pembe ya Afrika.

Kauli hiyo, ilitolewa na Rais wa Tume ya Umoja huo, Moussa Faki Mahamat, baada ya viongozi kutoka mataifa ya IGAD, kukutana nchini Djibouti, mwishoni mwa wiki, kujadiliana kuhusu mvutano huo.

Hayo yanajiri wakati Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, akikutana ana kwa ana na mwenzake wa Somalia, Mohamed Abdullahi, ambaye wiki iliyopita, alivunja uhusiano na Kenya.

Somalia inadai kuwa nchi hiyo inaingilia siasa zake za ndani kuelekea uchaguzi mkuu, mwaka ujao, madai ambayo Kenya imekanusha.

Siku ya Jumatatu, Rais Kenyatta alikutana na kufanya mazungumzo na rais wa jimbo linalojitegemea na ambalo lilitangaza kujitawala la Somaliland, Muse Bihi Abdi.

Uongozi wa Mogadishu, pia umekuwa ukiishtumu Kenya kwa kumuunga mkono Rais wa Jimbo la Jubaland, Ahmed Madobe, ambaye ana uhusiano mzuri na rais wa nchi hiyo, Mohamed Abdullahi Farmajo.

Mzozo huo unajiri wakati huu nchi hizo zikiendelea kutegemeana katika masuala ya kiuchumi pamoja na usalama, kutokana na Jeshi la Kenya, KDF, kuwa nchini Somalia kusaidia katika vita dhidi ya kundi la kigaidi la Al Shabab..

***RFI***

# Upinzani Jamhuri ya Afrika ya Kati walalama

**Bangui, CAR**

MUUNGANO wa upinzani kwenye Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR), mwishoni mwa wiki, uliomba uchaguzi uliopangwa kufanyika Desemba 27, mwaka huu, usitishwe.

Ulitaka usitishwe kutokana na ghasia kutoka kwa makundi ya wapiganaji, zinazoendelea nje ya mji mkuu wa Bangui, ingawa serikali ilisema ni lazima zoezi hilo liendelee kama ilivyopangwa.

Jumamosi iliyopita, serikali ilimlaumu aliyekuwa Rais wa Taifa hilo, Francois Bozize kwa kupanga kupindua serikali baada ya kunyimwa nafasi ya kuwania kiti cha urais.

Kwa mujibu wa shirika la habari la Reuters, mapigano yamekuwa yakiendelea kwenye miji kadhaa, ukiwamo ule wa Mbaiki, ulioko takriban kilomita 100 kutoka Bangui.

Muungano wa upinzani unaojulikana kama Cod2020, na ambao Bozize ni mwanachama unadai kuwa, ghasia zimezuia wagombea wa urais na ubunge, kufanya kampeni zao.

Wanasema kuwa vifaa muhimu vya kampeni pia vimeharibiwa kwenye ghasia hizo, wakati pia kukiwa na madai ya kutishiwa maisha.

Kupitia taarifa ya pamoja wamesema kuwa zoezi la uchaguzi haliwezi kufanyika kamwe kwa mazingira yaliyopo nchini.

***VOA***

# Kenya yadai itawafuta kazi madaktari

**Nairobi, KENYA**

MADAKTARI nchini Kenya, wanaofanya kazi kwenye hospitali za umma wameungana na wahudumu wengine kwenye mgomo, kulalamikia kutopewa bima ya afya na kufanya kazi kwenye mazingira magumu.

Wamesema mazingira ni magumu hasa katika kipindi hiki ambacho taifa hilo linapitia changamoto ya janga la virusi vya Covid-19.

Mgomo huo, unakuja baada ya mazungumzo kati ya wawakilishi wa madaktari na serikali nchini humo, kugonga mwamba.

Waziri wa Afya, Mutahi Kagwe, ametishia kuwafuta kazi wahudumu walioamua kugoma.

Mgomo huo, unakuja wakati huu nchi hiyo inapoendelea kukabiliana na janga la corona.

Kufikia sasa, Kenya imerekodi visa 94,500 vya maambukizi ya virusi vya corona, baada ya visa vipya 349 kuthibitishwa na vifo 94,500 baada ya watu wengine sita, kuthibitishwa kufariki dunia kutokana na COVID-19.

Watu 176, wameripotiwa kupona virusi hivyo na kufanya idadi ya jumla ya watu waliopona kufikia 75.

***RFI***



# BENZEMA NI MCHEZAJI WA KIPEKEE – ZIDANE

**MADRID, Hispania**

KARIM Benzema anacheza "kipekee" baada ya kusaidia tena Real Madrid kupata ushindi mwingine, amesema kocha Zinedine Zidane.

Benzema alifunga bao moja na kutoa pasi za mwisho mbili wakati Madrid wakipata ushindi wao wa tano mfululizo kwenye mashindano yote, baada ya kuichapa Eibar 3-1 kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Jumapili.

Ilikuwa ni kwa mara ya 30 mshambuliaji huyo wa Ufaransa kufunga na kutoa pasi za mwisho kwenye mchezo mmoja wa LaLiga.

Ni Cristiano Ronaldo pekee ndiye aliyemzidi, ambaye amefunga na kutoa pasi za mwisho kwenye mchezo mmoja (mara 44) kuliko mchezaji yeyote wa Madrid kwa karne ya 21.

Kiwango cha Benzema kilisifiwa na Zidane wakati Madrid wakifikisha pointi sawa na Atletico 29 kileleni mwa msimamo, ingawa vijana hao wa Diego Simeone wana mechi mbili mkononi.

"Ni mchezaji wa kipekee, lakini si tu kwenye goli," alisema Zidane akiwaambia waandishi wa habari.

"Si tu kwenye goli, ni kwenye mchezo mzima. Na ni mchezaji muhimu sana kwenye timu yetu."



# MOURINHO
## AKATAA KUWALAUMU WACHEZAJI

**LONDON, England**

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho, amekataa kumlaumu Serge Aurier kwa kusababisha penalti wakati wakichapwa mabao 2-0 nyumbani na Leicester City, Jumapili kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya England.

Spurs sasa wamepitwa pointi sita na vinara wa Ligi Kuu, Liverpool baada ya pia kupoteza kule Anfield.

Aurier alisababisha penalti kipindi cha kwanza kwa kumsukuma Wesley Fofana na ikafungwa na Jamie Vardy.

Baada ya James Maddison kufanya jitihaza zake za kutafuta bao la kusawazisha, lilikataliwa na VAR kwa madai kuwa aliotea, na mpira wa kichwa wa Vardy ukamgonga Toby Alderweireld na kuipa Leicester bao la pili.

Tottenham walishindwa kupata bao la kufutia machozi, huku macho ya mashabiki wake wengi yakiwa kwa Aurier, ambaye siku za hivi karibuni amekuwa akifanya makosa ya mara kwa mara.

Aurier amesababisha penalti nne tangu msimu wa Ligi Kuu England wa 2017-18 na ni David Luiz pekee ndio amesababisha penalti nyingi (5).

Hata hivyo, Mourinho aliwaambia waandishi wa habari: "Ni tatizo? Ngoja tujikite na yajayo.

"Lilikuwa kosa, lakini lilikuwa kosa dakika ya 45 au 46. Halafu tukawa na wachezaji wakifanya makosa sehemu nyingine. Siwezi kuwalaumu wachezaji kwa kufanya makosa.

"Penalti si kwamba ni penalti tuliyoitengeneza. Ni penalti ambayo tulihusika nayo. Si kitu cha kutengeneza, huwa inatokea kwa makosa yetu.

"Tulianza vibaya. Dakika 20 za mwanzo tulicheza katika kiwango kibaya, tulikuwa na nafasi nyingi lakini hatukucheza kwa bidii na kujituma."

# PIOLI AKUNWA LEAO KUBEBA MIKOBA YA IBRAHIMOVIC

**MILAN, Italia**

STEFANO Pioli anasubiri kwa hamu kurudi dimbani kwa mshambuliaji Ibrahimovic, lakini kocha huyo wa AC Milan alifurahishwa mno na kiwango cha Rafael Leao kwenye mchezo dhidi ya Sassuolo.

Leao alifunga bao la haraka zaidi kwenye historia ya Serie A - baada ya kutikisa nyavu sekunde ya sita - wakati Milan wakiibuka na ushindi wa 2-1 dhidi ya Sassuolo, Jumapili.

Milan ilirudi kwenye mtindo wake wa kushinda baada ya kupata sare mfululizo, na wanaongoza kwa pointi moja dhidi ya wapinzani wao, Inter waliopo nafasi ya pili kwenye msimamo.

Vijana hao wa Pioli wameendelea kukaa kileleni mwa msimamo wa Serie A bila kupotea mchezo wowote kati ya 13 licha ya Ibrahimovic kutokuwapo tangu Novemba - ambapo straika huyo amefunga mabao 11 msimu huu - akiwa nje ya dimba kwa mwezi mmoja kutokana na kuumia kigimbi.

Licha ya kikosi hicho kumkosa straika huyo mwenye umri wa miaka 39, Pioli anaamini Ibrahimovic atarudi hivi karibuni.

"Kitu cha kwanza, tukiwa na Ibra tunakuwa timu imara zaidi. Yeye ni bingwa na kwa uwapo wake tumekuwa timu imara," alisema akiwaambia waandishi wa habari."

Leao mwenye umri wa miaka 21, ni mchezaji mwenye umri mdogo zaidi ambaye amekuwa na mabao matatu kwenye ligi kubwa tano za Ulaya kwa kila msimu kwa misimu mitatu mfululizo.

Alexis Saelemaekers alifunga bao la pili kwa Milan licha ya Domenico Berardi kufunga la kufuatia machozi kwa Sassuolo.

"Nina furaha kubwa na Leao kwa sababu kuna wakati namtaka afanye mengi zaidi kuliko uwezo wake," amesema Pioli.

HABARI MICHEZO



# CONTE ATAKA KIWANGO ZAIDI INTER MILAN

**MILAN, Italia**

ANTONIO Conte amesema anachoangalia zaidi kwa sasa ni mwendelezo wa kiwango bora kwa Inter Milan, kuliko matokeo ya mchezo mmoja, baada ya timu hiyo kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Spezia.

Sasa Inter imeshinda mechi sita mfululizo za Ligi Kuu ya Italia, Serie A msimu huu.

Inter ilianza kwa kusuasua kwenye mchezo huo uliopigwa Uwanja wa San Siro na kutengeneza nafasi chache, huku Spezia iliyopanda daraja msimu huu ikiwa na umiliki mkubwa zaidi wa mpira.

Lakini Achraf Hakimi alifunga bao la kwanza mwanzoni mwa kipindi cha pili na Romelu Lukaku akafunga kwa penalti na kuwaacha Spezia hawana cha kufanya.

Hii ni mara ya nne kwa Inter kushinda mechi nne mfululizo kwenye Serie A nyumbani chini ya Conte.

Na Conte alifurahishwa na matokeo hayo ya Inter, lakini alisema anachoangalia zaidi ni mwendelezo wa kiwango cha 'Nerazzurri' hao.

"Tumeshinda mechi sita mfululizo na tunaukaribisha ushindi huu, kwa sababu kama unakuwa na mwendelezo wa kiwango bora, mambo yanakwenda kwa urahisi tu," alisema akiiambia Sky Sport Italia."

# SOLSKJAER AMSIFU MCTOMINAY AKIWEKA REKODI EPL

**MANCHESTER, England**

OLE Gunnar Solskjaer amepaza sauti kusifia "nguvu na ufiti" wa Scott McTominay baada ya kiungo huyo wa Manchester United kuweka rekodi kwenye historia ya Ligi Kuu England, wakati wakiifumua Leeds United.

Man United waliwafunga Leeds mabao 6-2 kwenye dimba la Old Trafford, huku mabao mawili ya kwanza yakipatikana ndani ya dakika tatu. McTominay alifunga yote hayo, yakiwa ya haraka zaidi kwenye mashindano hayo, wakati United wakiwa kwenye ubora wao.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Scotland pia alitoa pasi ya mwisho kwa Daniel James aliyefunga bao la tano moja kati ya nafasi tatu ilizotengeneza.

Ingawa McTominay alitolewa kutokana na maumivu ya nyonga, Solskjaer alimnyooshea kidole kiungo huyo alivyoonyesha kuwa na nguvu kubwa zaidi.

"Tulijua kwamba walikuwa kwenye ari kubwa na tulitakiwa kucheza kwa tahadhari," alisema kocha huyo.

"Lakini kiukweli kabisa McTominay ameonyesha ana nguvu ya ziada na ari kubwa zaidi mbele ya bao na kasi kubwa zaidi.

"Ana nguvu. Alifanya kazi kubwa, kila siku anafanya mazoezi ya nguvu. Anaonyesha kwamba ataendelea kuwa fiti zaidi."



# TUCHEL ALALAMIKIA RATIBA PSG IKIPOTEZA WATATU

**PARIS, Ufaransa**

THOMAS Tuchel ameonya kwamba ratiba ya sasa "itawaua wachezaji" baada ya Paris Saint-Germain kukumbana na majeruhi wengine watatu, wakati wakitoka suluhu kwenye mchezo wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, dhidi ya Lille.

Tuchel tayari alikuwa na majeruhi wengine wakati akienda kupambana na Lille pale kwenye dimba la Pierre-Mauroy, akiwakosa Neymar na Mauro Icardi.

Kylian Mbappe pia hayupo fiti, hakucheza kwa dakika nyingi katika siku yake ya kuazimisha kuzaliwa akitimiza umri wa miaka 22, huku mabingwa hao wa Ufaransa wakishinda kupaa kileleni mwa msimamo.

Lakini PSG ikawapoteza Presnel Kimpembe, Alessandro Florenzi na Layvin Kurzawa kwenye mchezo huo wa Jumapili, hivyo watakuwa na wakati mgumu wakati watakapowakabili Strasbourg, Jumatano.

Tuchel alizungumzia ratiba ilivyo ngumu kwao huku wakiachwa wakipitwa pointi moja na vinara Lille na Lyon waliopo nafasi ya pili.

Baada ya mchezo huo wa sare, aliiambia Telefoot: "Tayari mnajua mawazo yangu, tutawaua wachezaji.

"Mara zote tumekuwa tukicheza saa 3 usiku. Tunakosa ubora wetu wa kula, kulala na kupumzika. Lakini itaendelea kwa mtindo huu.

"Leo (juzi) tumewakosa Neymar, Kylian, Mauro, Juan (Bernat). Tunashangaa? Hapana. Kuna wachezaji wapya tena wameumia. Ndivyo wanavyotaka."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# LIVERPOOL KUMUUZA SALAH – ABOUTRIKA

●●●Hana furaha pale Anfield, aliniambia sababu, lakini ni siri siwezi kuitoa hadharani...

**LIVERPOOL, England**

MOHAMED Salah hana furaha Liverpool na miamba hao wa Ligi Kuu England wanafikiria kumuuza nyota huyo, kwa mujibu wa mchezaji mwenzake wa zamani wa timu ya Taifa ya Misri, Mohamed Aboutrika.

Salah, ambaye ameng'ara tangu kutua pale Anfield mwaka 2017, alikataa kuondoa uwezekano wa kuhamia Real Madrid au Barcelona wakati wa mahojiano yake ya hivi karibuni na AS.

Mshambuliaji huyo pia alisema alikatishwa tamaa kwa kutopewa kitambaa cha unahodha kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati Liverpool wakiwavaa Midtjylland mapema mwezi huu.

Aboutrika, ambaye amecheza mechi 100 kwa Misri, amesema Salah hana furaha pale Liverpool.

"Nilimpigia simu Salah kuhusu hali yake pale Liverpool na alionekana kabisa hana raha, lakini hilo haliwezi kuathiri kiwango chake dimbani," alisema akiambia beIN SPORTS.

"Najua kwamba, Salah hana furaha pale Liverpool, aliniambia mimi sababu ya yeye kutokuwa na furaha, lakini ni siri na siwezi kuzungumza hadharani.

"Moja ya sababu iliyomfanya Salah akasirike ni kushindwa kupewa unahodha kwenye mchezo dhidi ya Midtjylland."

Salah alijiunga na Liverpool akitokea AS Roma kwa ada iliyoripotiwa kuwa pauni milioni 36.9 katikati ya mwaka 2017. Aboutrika anaamini mabingwa hao wa Ligi Kuu England wanafikiri kuhusu kumuuza straika huyo mwenye umri wa miaka 28.

"Kwa mawazo yangu, Liverpool wanafikiria kumuuza Salah kwa sababu ya kiuchumi," alisema.

Salah amefunga mabao 110 katika mechi 173 alizocheza pale Liverpool, yakiwamo 16 katika mechi 21 msimu huu.

Ameisaidia klabu hiyo kushinda taji la Ligi Kuu England, Ligi ya Mabingwa Ulaya, UEFA Super na Klabu Bingwa Dunia.

## KWA UFUPI

**BISSOUMA AWANIWA UNITED**

MANCHESTER United inamwania nyota anayewaniwa pia na Liverpool na Arsenal, Yves Bissouma kutoka Brighton mwenye umri wa miaka 24 raia wa Mali, ambaye msimu huu umekuwa wa kuvutia kwake. ***(Express)***

**MARSEILLE WAMTAKA GIROUD**

KLABU ya Marseille inataka kumsajili mshambuliaji wa Chelsea raia wa Ufaransa, Olivier Giroud mwenye umri wa miaka 34. ***(le10sport)***

**MADRID IMANI KWA MBAPPE**

REAL Madrid inajiamini sana kumsajili straika wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22, kipindi cha majira ya joto kijacho, kutoka kule Paris St-Germain. ***(90 Min)***

**ALABA ANAONDOKA BAYERN**

MWENYEKITI wa Bayern Munich, Karl-Heinz Rummenigge, amekubali kwamba, mlinzi David Alaba mwenye umri wa miaka 28, anapanga kuondoka klabu hiyo ya Ujerumani. Mkataba wa sasa wa raia huyo wa Austria unamalizika Juni 30, mwakani, na mchezaji huyo anaweza kufanya mazungumzo na klabu yoyote kuanzia Januari Mosi, huku Real Madrid ndiyo ikionekana sehemu anayoweza kutua. ***(Marca)***

**KEANE NA UBINGWA EPL**

KIUNGO wa zamani Manchester United, Roy Keane, anaamini klabu hiyo ndio timu itakayotoa changamoto kubwa zaidi kwa Liverpool kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu msimu huu. ***(Sky Sports)***

**DYBALA HAONDOKI JUVE**

KOCHA wa Juventus, Andrea Pirlo amekanusha uwezekano wa mshambuliaji wa Argentina, Paulo Dybala mwenye umri wa miaka 27 kuondoka klabuni hapo. ***(Mail)***

**CITY KUMUUZA ZINCHENKO**

KLABU ya Manchester City inafikiria kusikiliza ofa kwa mlinzi wake wa kimataifa wa Ukraine, Oleksandr Zinchenko mwenye umri wa miaka 24, wakati wa dirisha dogo la Januari. ***(Express)***

**RUDIGER HANA RAHA CHELSEA**

MLINZI wa Ujerumani, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 27, amekubali "haridhishwi" na hali yake ya sasa pale Chelsea, lakini amesisitiza hatatafuta timu ya kujiunga nayo wakati wa dirisha la Januari. ***(ZDF via Mail)***

**KUBO KUONDOKA VILLARREAL**

WINGA wa kimataifa wa Japan, Takefusa Kubo mwenye umri wa miaka 19, anaweza kumaliza kipindi chake cha kucheza kwa mkopo wa muda mrefu pale Villarreal Januari baada ya kukosa namba chini ya kocha, Unai Emery. ***(As)***

**BECKHAM AMTAKA ROMERO**

KLABU inayomilikiwa na David Beckham ya Inter Miami inayoshiriki Ligi Kuu Marekani, MSL, imeendelea kuonyesha nia ya kuhitaji huduma ya kipa wa Manchester United, Sergio Romero mwenye umri wa miaka 33, huku raia huyo wa Argentina akitaka kuondoka pale Old Trafford. ***(Express)***



HABARI MICHEZO

# MKWASA ATOA SIRI RUVU KUKIMBIZA LIGI KUU BARA

**Na Saada Akida**

HUKU akisubiri kumaliza mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Namungo FC, Kocha Mkuu wa Ruvu Shooting, Boniface Mkwasa, amesema kutoa nafasi ya kucheza kwa vijana ndiyo siri kubwa ya kufanya vizuri msimu huu.

Ruvu Shooting ipo katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 25 baada ya mechi 16, ikishinda sita na sare saba huku ikipoteza mechi tatu pekee.

Katika mechi iliyopita dhidi ya Azam FC iliyopigwa Ijumaa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam, Ruvu Shooting iliambulia sare ya mabao 2-2.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam, Mkwassa alisema amekuwa akiwatumia wachezaji vijana katika mechi za ligi hiyo ambao wanakasi na wako fiti kwa ajili ya kukabiliana na wapinzani wao.

Alisema ligi imekuwa na ushindani mkubwa sana, na kila mechi unatakiwa kuwa na mbinu tofauti ili kuhakikisha wachezaji wanakuwa fiti na kuongeza kasi ya kupambana, jambo ambalo vijana wake wamekuwa wakilionyesha.

Mkwasa alisema malengo yake makubwa ni kumaliza ligi hiyo wakiwa katika nafasi tano za juu huku akidai ubingwa wanawaachia Simba, Yanga na Azam FC.

"Hata wachezaji wakihitaji kucheza mpira basi waje Ruvu Shooting, ila kama wanataka mamilioni ya fedha basi waende katika klabu hizo," alisema Mkwassa.

Yanga ndiyo iliyopo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama 40 baada ya kushuka dimbani mara 16 sawa na Azam FC iliyopo nafasi ya tatu na alama zake 29, huku Simba ambayo ipo mechi mbili nyuma, ikiwa na pointi 32 katika nafasi ya pili.

Ligi hiyo inatarajiwa kuendelea leo kwa kupigwa mechi nne ambapo Gwambina FC ya Miungwi, Mwanza itakuwa nyumbani kuikaribisha Mbeya City, huku Biashara United ya Mara nayo ikiwa mwenyeji wa Tanzania Prisons.

Kagera Sugar itakuwa katika uwanja wake wa Kaitaba mjini Bukoba kuikaribisha Polisi Tanzania wakati Mwadui FC ya Shinyanga ikiwa mwenyeji wa Coastal Union ya Tanga.

Kesho kutwa, Jumatano, zitapigwa michezo mitatu, ambapo JKT Tanzania itakuwa mwenyeji wa KMC FC huku Ihefu FC ikiwaalika vinara wa ligi hiyo, Yanga katika Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya na Mtibwa Sugar ikiwakaribisha Dodoma Jiji.

## Chuoni yaanza kuchonga Ligi Kuu Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya kuona 'mwezi' Ligi Kuu Zanzibar kwa kuifurumusha mabao 3-2 timu ya Polisi, Kocha Mkuu wa Klabu ya Chuoni, Ali Bakar Mngazija, ameanza 'kuchonga' kwa kueleza kuwa ushindi huo ni mwanzo wa kuhakikisha wanafanya vizuri kutokana na kuvurunda katika michezo minne ya mwanzo.

Ushindi huo iliyoupata kwenye Uwanja wa Amaan juzi, ni wa kwanza kwa Chuoni katika michezo mitano iliyocheza hadi sasa, ambao unaifanya kufikisha pointi nne, hivyo kushika nafasi ya pili kutoka mkiani kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 12 msimu huu.

Mabao ya Chuoni katika mchezo huo yalifungwa na Ali Khamis dakika ya 11, Mustafa Zakaria dakika 36 na Mundhir Abdallah dakika ya 50, huku yale ya Maafande wa Polisi yakifungwa na Suleiman Ali dakika ya 30 na Ali Khatib dakika ya 57.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mechi hiyo, Kocha Mkuu wa Chuoni FC, Mngazija, alisema ushindi wa mchezo huo ni mwanzo wa kuhakikisha timu hiyo sasa inaanza kufanya vizuri katika mechi zijazo.

Alisema amefanyia kazi mapungufu mengi yaliyokuwapo awali kwa kuongeza umakini kwa wachezaji hususan washambuliaji kuhakikisha wanatumia nafasi wanazozipata.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Polisi, Yusuph Sape, alisema kupoteza mchezo huo dhidi ya Chuoni ni kutokana na timu yake kuzidiwa kipindi cha pili.

Hata hivyo, alisema kwa sasa anaelekeza nguvu zake katika mchezo wake dhidi ya timu ya Hard Rock ambao watakuwa ugenini, Kisiwani Pemba kesho, Jumatano katika Uwanja wa Gombani.

KANITANGAZE...




Mwekezaji na Mwenyekiti wa Bodi ya Simba, Mohammed 'Mo' Dewji ameendelea kuitangaza klabu hiyo kimataifa baada ya jana kuposti picha ya beki wa kati wa Barcelona, Gerard Pique, akiwa ameshika jezi ya klabu hiyo na kuambatanisha na ujumbe: "Ni fahari kuweza kujenga uhusiano na mchezaji wa aina yake. Tunaamini kuna mengi ambayo tutaweza kujifunza na atakayotushauri yatakayoleta maendeleo ya mpira hususan kwa vijana".

## Azam yatapatapa kuvurunda Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

HUKU taarifa zikiendelea kusambaa kupitia mitandao ya kijamii kuwa kuvurunda kwa Azam FC kumetokana na uongozi kupunguza posho za wachezaji, klabu hiyo imeibuka na kukanusha.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thabit Zacharia, amesema si kweli kwamba wamepunguza posho, badala yake imeongezeka zaidi msimu huu.

Kutokana na timu hiyo kutofanya vema kwa takriban mechi sita, kuna uvumi unaenezwa kwenye baadhi ya mitandao ya kijamii kuwa uongozi wa klabu hiyo umepunguza posho kwa wachezaji ndiyo maana wamekuwa hawajitumi.

"Kwanza kabisa ni habari za kupuuzwa, kimsingi si taarifa za kweli, hatujapunguza posho ila zimeongezeka. Ni kwamba posho za msimu uliopita zimebaki vile vile zilivyo. Lakini msimu huu kuna posho zingine zimeongezwa, kwani kuna kipengele kingine kuwa timu ikishinda mechi tatu mfululizo, basi kuna posho yake pia kwa wachezaji, ukiacha ile ya msimu uliopita ambayo iko pale pale timu ikishinda tu mechi moja ya ligi," alisema Zacharia. Alisema kwa maana hiyo jukumu sasa linabaki kwa wachezaji washinde ili wapate posho zao.

Azam imecheza mechi sita mfululizo bila kupata ushindi tangu ilipoichapa Dodoma Jiji mabao 3-0 Novemba 5, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex.

## ZFF yatoa darasa usajili kwa mtandao

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limeendelea kutoa elimu ya usajili kwa njia ya mtandao kwa klabu za Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja visiwani hapa.

Kuanzia msimu huu klabu zote zinazoshiriki ligi katika ngazi mbalimbali visiwani Zanzibar zinatakiwa kutumia kusajili kwa njia ya mtandao ikiwa ni pamoja kutangaza orodha ya wachezaji watakaoanza na wakukaa benchi katika mchezo husika, ambapo hapo awali elimu hiyo ilitolewa kwa klabu zote 12 za Ligi Kuu Zanzibar msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili juzi, Mkurugenzi wa Mashindano wa ZFF, Ali Mohammed Ameir, alisema licha ya kuendelea kutoa elimu ya matumizi ya mfumo mpya wa usajili wa wachezaji, lakini bado kuna changamoto kwa baadhi ya klabu. 'Utakuta mchezaji katika mfumo kawekwa jezi labda namba 10, lakini uwanjani anapewa jezi namba nyingine hapa kunakuwa na mkanganyiko hususan mchezaji anapofanya makosa, au hata akifunga bao, pia katika kujaza ripoti katika mfumo huu utakuta mhusika ni mwingine," alisema.

Hata hivyo, alisema wanaendelea kuwafahamisha waamuzi pia kuhakikisha orodha inayotolewa na ZFF isibadilishwe pindi inapofika uwanjani ili kuondoa mkanganyiko unaojitokeza.

# Michezo

Jumanne Desemba 22, 2020

Nipashe




## LIVERPOOL KUMUUZA SALAH – ABOUTRIKA

HABARI UK 22

SIKU YETU...



Mshambuliaji wa Manchester United, Anthony Martial, akijaribu kufunga bila mafanikio huku akiwa amezungukwa na msitu wa mabeki wa Leeds United wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 6-2 kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Old Trafford juzi. **HABARI UK. 21**

# BOCCO, MANULA HATIHATI KUIVAA PLATINUM KESHO

## ●●●Bado majeruhi, Lwanga naye ITC haijafika, Barbara afunguka majembe kutoka Nigeria...

**Na Adam Fungamwango**

NAHODHA na mshambuliaji wa Klabu ya Simba, John Bocco na kipa namba moja wa timu hiyo, Aishi Manula, wapo kwenye hatihati ya kuivaa FC Platinum katika mechi ya kwanza ya raundi ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika inayotarajiwa kupigwa Uwanja wa Taifa wa Zimbabwe kesho, imeelezwa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo (CEO), Barbara Gonzalez, amesema wachezaji hao bado ni majeruhi, lakini kwa sasa wanaendelea na matibabu na hali yao imefikia hatu nzuri.

Wachezaji hao walitolewa kwa nyakati tofauti kwenye mechi ya Ligi Kuu kati ya timu hiyo na KMC FC, Simba ikishinda kwa bao 1-0, ambapo nafasi ya Manula ilichukuliwa na Beno Kakolanya na ya Bocco ikitwaliwa na Chris Mugalu.

Barbara alisema hayo akiwa nchini Zimbabwe wakati wa mahojiano ya moja kwa moja na waandishi wa habari kuelekea mchezo huyo wa kwanza wa raundi ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Bocco na Aishi bado wanaendelea na matibabu, kwa sasa wamefikia kwenye hatua nzuri na Mwenyezi Mungu atawawezesha wapone. Na tunawaomba mashabiki wetu wawaombee, wawaweke kwenye dua zao ili wapone haraka waweze kucheza mechi hiyo," alisema Barbara.

Kwa maana hiyo kuna uwezekano wa kucheza au kutocheza wachezaji hao kwenye mechi ya kesho, na hiyo itategemea na jinsi watakavyopona na kuwa tayari kwa mchezo huo.

Barbara pia alisema mpaka sasa klabu yao haijapata uhamisho wa kimataifa (ITC) kutoka nchini Misri wala barua ya kuipa ruhusa klabu hiyo kumtumia kiungo Mganda Taddeo Lwanga kutoka Klabu ya Tanta, lakini wamekuwa kwenye harakati ya kuhakikisha kila kitu kinapatikana ndani ya siku hizi mbili zilizobaki (jana na leo).

Kuhusu maandalizi, alisema kuwa kila kitu kimekamilika na wachezaji wako tayari kupambana.

Aidha, Barbara amekanusha kuhusu klabu yao kutaka kumsajili mchezaji Justine Songa, Mzambia anaichezea Orlando Pirates ya Afrika Kusini.

"Hata mimi nimeona kwenye mitandao ya kijamii, hamna kitu, hayupo kwenye mipango yetu na hata kwenye kamati ya usajili jina lake halipo katika mapendekezo," alisema.

Kuhusu usajili, Barbara alisema kuwa Simba ipo mbioni kusajili baadhi ya wachezaji hasa kwenye kipindi hiki cha dirisha dogo, huku wengine ikitarajia kuwatoa kwa mkopo kwenda klabu mbalimbali.

"Ndiyo, tuna wachezaji tumekuwa tukiwaangalia kutoka Nigeria kama wanaweza kutufaa na sehemu nyingine mbalimbali. Kuna wengine watasajiliwa watacheza pia ligi, Shirikisho la Soka Afrika (CAF), lilituruhusu kusajili wachezaji, lakini Shirikisho la Soka nchini (TFF), lilituambia kuwa watakaozidi basi hawatocheza ligi ya ndani, watatumika tu kwenye mechi za kimataifa, kwa hiyo yote tumeyazingatia. Lakini kwa wale tutakaowatoa kwa mkopo sitoweza kuwataja majina hapa kwa sasa, ila wapo watakaoondoka," alisema Barbara mwanamke pekee Ofisa Mtendaji Mkuu kwa klabu za soka Afrika Mashariki.

# NTIBAZONKIZA SASA AUTAJA UBINGWA YANGA SC

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI mashabiki wakitarajia kuona ingizo jipya ndani ya Klabu ya Yanga, Mrundi Saidi Ntibazonkiza, akianza katika kikosi cha kwanza kesho dhidi ya Ihefu FC, mshambuliaji huyo ameutaja ubingwa wa Ligi Kuu Bara.

Yanga itashuka katika Uwanja wa Sokoine kesho kukamilisha raundi ya kwanza ya Ligi Kuu ikitoka kuvuna alama tatu dhidi ya Dodoma Jiji FC kwenye Dimba la Sheikh Amri Abeid jijini Arusha baada ya Jumamosi iliyopita kushinda 3-1 wakati wenyeji wao, Ihefu wenye siku hiyo waliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya KMC FC.

Katika mchezo huo, Ntibazonkiza aliyeingia kipindi cha pili akitokea benchi, alikuwa sehemu ya ushindi baada ya kufunga bao moja na kumtengenezea lingine Bakari Mwamnyeto.

Hata hivyo, kuelekea mchezo dhidi ya Ihefu, ambao kuna uwezekano mkubwa Kocha wa Yanga, Cedric Kaze, kumwanzisha, amesema anatamani kuona timu yake hiyo ikitwaa ubingwa na yeye kuwa sehemu ya mafanikio hayo.

"Wakati nakuja hapa sikufahamu kiundani nitakutana na watu wa aina gani, nimehamasika sana baada ya kukuta kila mtu ndani ya Yanga analia na ubingwa, ndiyo maana katika kila mchezo wachezaji hujitolea hadi mwisho.

"Hilo limenifanya hata mimi sasa kutamani kuipa Yanga ubingwa, Mungu akipenda msimu huu tutakuwa mabingwa," alisema.

Yanga ipo kieleleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 40 baada ya mechi 16, ikifuatiwa na Simba yenye alama 32 zilizotokana na michezo 14, wakati Azam FC ikishika nafasi ya tatu kwa pointi 29 kutokana na kushuka dimbani mara 16.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042